# ATHARI ZA KIISIMU ZA LAHAJA YA KITUMBATU KATIKA KISWAHILI SANIFU KINACHOTUMIKA KATIKA SHULE ZA TUMBATU ZANZIBAR

**PANDU MACHANO AME**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI - ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma na anapendekeza tasnifu hii inayohusu ***athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar***, ipokelewe na ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha matakwa ya kuhitimu shahada ya uzamili wa Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……..……

Dkt. Anna Kishe

( Msimamizi)

…….

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote, sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya ruhusa ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi,**Pandu Machano Ame,**natamka kuwa kazi hii yenye jina "*Athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar"*ni yangu mwenyewe, haijawahi kuwasilishwa popote kwa lengo la kufaulu shahada kama hii.

…….....

Sahihi

……..

Tarehe

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa, marehemu Machano Ame Juma na Fatuma Moh’d Yussufu kwa kunilea katika malezi bora na katika misingi bora ya kitaaluma ya kidini na kidunia. Pia ninaitabaruku kwaMke wangu Mariamu Habibu Bakari kwa kunipa ushirikiano mzuri katika maisha yanguna katika kipindi cha masomo.

## SHUKURANI

Watu waliotoa michango yao hadi kumalizika kwa kazi hii ni wengi sana na ni vigumu kuwataja wote, ila ninawaomba waamini kuwa michango yao imepokelewa kwa moyo mkunjufu na imesaidia kufanikisha kazi hii. Ninawaomba radhi sana kwa kutowataja ila Mungu awajaze imani na Baraka katika misha yao. Hata hivyo ninapenda kuwataja wachache kwa niaba yao.

Kwanza kabisa ninatoa shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyenipa uhai, nguvu, fikra na uwezo wa kuandika na kukamilisha kazi hii.

Pili, ninatoa shukrani za pekee kwa msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt, Anna Kishe kwa kukubali kubeba jukumu la kusimamia kazi hii, ninamshukuru kwa ujasiri, upendo na uvumilivu wake mkubwa tokea hatua ya kuandika pendekezo la utafiti hadi kumalizika kwa kazi hii. Ni imani yangu kwamba amevumilia sana kutokana na udhaifu wangu wa kibinaadamu na uanafunzi. Mafanikio ya tasnifu na juhudi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha, kuelekeza na kushauri yale yote yanayofaa kuzingatiwa katika utafiti huu. Pamoja na majukumu mengi aliyonayo, hakusita hata mara moja kusoma kazi yangu kwa umakini mkubwa. Kwa kweli sina kitu cha kumlipa ila ninamuombea dua kwa Mwenyezi Mungu amzidishie upendo, ampe afya njema, ampe maisha marefu yenye kheri ili aweze kutoa mchango kwa wanataaluma na taifa kwa ujumla.

Tatu, ninapenda kuushukuru uongozi wa chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na idara ya isimu na taaluma za fasihi kwa kuanzisha shahada ya uzamili ya Kiswahili na kunichagua mimi kuwa ni mmoja kati ya wanafunzi wa isimu waliochaguliwa

kujiunga na Chuo hiki.shukurani za dhati ziwafikie wahadhiri wote ambao waliweza kuacha familia zao na kusafiri hadi hapa Zanzibar ili kutupatia taaluma ya kozi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa upendo, awape afya njema na maisha marefu ili waendelee kutoa mchango wa kitaaluma katika taifa letu.

Nne, ninatoa shukurani kwa wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya uzamili wa Kiswahili wa mwaka wa masomo 2015/ 2016 kutokana na mashirikiano yao ya dhati katika masuala ya kitaaluma kwa kipindi chote cha masomo.

Tano, ninatoa shukurani kwa viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali kwa kuniruhusu kutumia maktaba zao katika kujipatia taaluma iliyojisaidia kukamilisha kazi hii. Pia ninawashukuru sana viongozi wa shule za Tumbatu, walimu na wanafunzi wao wote kwa mchango wao mkubwa walionipatia hasa kwa kukubali kuwa watafitiwa na kuweza kunipatia taarifa zilizoweza kunisaidia kukamilisha kazi hii.

Mwisho, ninatoa shukrani za dhati kwa mama mzazi kwa malezi yake mazuri, pia mke wangu na watoto wangu kutokana na uvumilivu mkubwa waliouonesha katika kipindi changu chote cha masomo hasa wakati ambapo nililazimika kuwa mbali nao. Vile vile ninawashukuru sana kaka zangu na dada zangu kwa kunitaka kuwa na subra na kuzidisha bidii katika masomo hayo. Wote hao ninawaambia ahsante sana.

## IKISIRI

Utafiti huuumejadili "*Athari za Kiisimu za Lahaja za Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika Katika Shule za Tumbatu Zanzibar".*Utafiti ulifanyika Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja na uliongozwa na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano. Nadharia hiyo ilianzishwa na Howard (1973) ambayo lengo lake kuu ni kueleza sababu za kubadili mtindo wa matamshi wakati wa mawasiliano wa kijamii na kuangalia athari zake katika jamii. Katika utafiti huu, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji, usaili na uchunguzi shirikishi. Jumla ya watafitiwa walikuwa 68. Miongoni mwao walimu walikuwa 29, na wanafunzi walikuwa 39. Vilevile utafiti huu umeonesha matokeo. Miongoni mwa matokeo hayo ni kwamba lahaja ya Kitumbatu baadhi ya wakati maumbo ya maneno hutumia ulahaja. Pia, lahaja ya Kitumbatu hudondosha viambishi katika maneno.Mwisho, sura imehitimisha kwa kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia wanajamii kufanya tafiti kwa za lahaja mbalimbali kwa lengo la kuweka kumbukumbu kwa vizazi vya baadaye.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ..... **ii**

**HAKIMILIKI** ..... **iii**

**TAMKO** ..... **iv**

**TABARUKU** ..... **v**

**SHUKURANI** ..... **vi**

**IKISIRI** ..... **viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **xiii**

**ORODHA YA VIAMBATANISHO** ..... **xiv**

**SURA YA KWANZA** ..... **1**

**UTANGULIZI** ..... **1**

1.1 Utangulizi kwa Jumla ..... 1

1.2 Usuli waTatizo ..... 2

1.3 Tatizo la Utafiti ..... 4

1.4 Malengo ya Utafiti ..... 5

1.4.1 Lengo Kuu ..... 5

1.4.2 MalengoMahususi ..... 5

1.5 Maswali ya Utafiti ..... 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 6

1.7 Mipaka ya Utafiti ..... 6

1.8 Maadili ya utafiti ..... 6

1.9 Hitimisho ..... 7

**SURA YA PILI ..... 8**

**MAPITIO YA KAZI Tangulizi na mkabala wa Nadharia ..... 8**

2.1 Utangulizi ..... 8

2.2 Maandiko kuhusu Kiswahili Sanifu ..... 8

2.3 Tafiti Zinazozungumzia Athari za Lahaja katika Kiswahili ..... 9

2.4 Kazi Tangulizi Kuhusu Kitumbatu ..... 11

2.5 Pengo la Utafiti ..... 17

2.6 Mkabala wa Nadharia ..... 18

2.7 Hitimisho ..... 20

**SURA YA TATU ..... 21**

**MBINU ZA UTAFITI ..... 21**

3.1 Utangulizi ..... 21

3.2 Eneo la Utafiti ..... 21

3.3 Kundi Lengwa ..... 21

3.4 Sampuli na Usampulishaji ..... 22

3.4.1 Sampuli. ..... 22

3.4.2 Mchakato wa Usamplishaji ..... 22

3.5 Mbinu za Utafiti ..... 23

3.5.1 Data ya Upili ..... 23

3.5.2 Data za Msingi ..... 24

3.5.2.1 Mbinu ya Usaili ..... 24

3.5.2.2 Mbinu ya Hojaji ..... 25

3.5.2.3 Mbinu ya Uchunguzishirikishi ..... 25

3.6 Zana za Utafiti..... 25

3.7 Hitimisho..... 26

**SURA YA NNE..... 27**

**UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ..... 27**

4.1 Utangulizi..... 27

4.2 Mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia Inayotokana na Lahaja ya Kitumbatu Iliyoathiri Kiswahili Sanifu ..... 28

4.2.1 Sauti za Kitumbatu..... 28

4.2.2 Mfumo wa Irabu katika Kitumbatu..... 28

4.2.2 Mfumo wa Konsonanti..... 30

4.3 Maumbo ya Maneno ya Kitumbatu..... 35

4.3.1 Maumbo ya Kitumbatu na Viambishi Vya Nafsi..... 35

4.3.2 Maumbo ya Maneno na Njeo..... 37

4.3.3 Maumbo ya Maneno ya Umilikishi ..... 39

4.3.4 Maumbo ya Maneno na Udondoshaji ..... 40

4.3.5 Maumbo ya Maneno Katika Uyakinishi na Ukanushi ..... 41

4.3.6 Maumbo ya Maneno na Mnyambuliko..... 42

4.3.7 Maumbo ya Ngeli za Nomino za Kitumbatu ..... 44

4.4 Tungo za Kitumbatu..... 47

4.4.1 Tungo katika Hali ya Kiima na Kiarifu ..... 47

4.4.2 Tungo za Kitumbatu na Upatanishi wa Kisarufi..... 48

4.5 Matumizi ya Lahaja ya Kitumbatu Darasani ..... 49

4.5.1 Matini za Walimu..... 49

4.5.2 Utungaji wa Insha ..... 50

4.6 Athari za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu ..... 53

4.6.1 Athari za kiisimu ..... 53

4.6.1.1 Athari Katika Sauti ..... 54

4.6.1.2 Athari katika maneno ..... 56

4.6.1.3 Athari katika Tungo ..... 60

4.6.1.3.1 Tungo Kirai ..... 60

4.6.1.3.2 Tungo Kishazi ..... 61

4.6.1.3.3 Tungo Sentensi ..... 62

4.6.2 Athari Katika Masomo Yanayofundishwa Shuleni ..... 64

4.6.3 Athari Katika Ujifunzaji ..... 65

4.6.4 Athari katika Ufundishaji ..... 66

4.7 Sababu zilizosababisha Athari Hizo katika Kiswahili Sanifu ..... 67

4.8 Hitimisho ..... 68

**SURA YA TANO ..... 69**

**MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 69**

5.1 Utangulizi ..... 69

5.2 Muhtasari wa Utafiti ..... 69

5.3 Matokeo ya Utafiti ..... 70

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ..... 73

5.5 Hitimisho ..... 74

**MAREJELEO ..... 75**

**VIAMBATANISHO ..... 79**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 3.1: Idadi ya Sampuli ya Watafitiwa ..... 22

Jedwali Na. 4.1: Mfumo wa Irabu za Kitumbatu ..... 29

Jedwali Na. 4.2: Konsonanti za Kitumbatu ..... 30

Jedwali Na 4.3: Athari za sauti katika Kitumbatu ..... 54

Jedwali Na 4.4: Athari za maneno katika Kitumbatu ..... 56

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho 1: Maswali ya Mtafiti kwa Walimu wa Somo la Kiswahili ..... 79

Kiambatanisho 2: Maswali ya Mtafiti kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari ..... 84

Kiambatanisho 3: Matini ya mwalimu wa somo la Kiswahili ..... 89

Kiambatanisho 4: Utungaji wa Insha kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekomdari ..... 90

Kiambatanisho 5: Maswali ya Mahojiano ..... 91

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizikwa Jumla

Sura hii imezungumzia historia fupi ya Tumbatu, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na maadili ya utafiti.

Tumbatu ni miongoni mwa visiwa vichache vinavyokaliwa na watu wa Zanzibar. Kisiwa hiki kipo Kaskazini Unguja kilomita 48 kutoka mjini unguja na kilomita 3 kutoka mkototoni. Kisiwa hiki kina urefu wa kilomita 15.5 na upana wa kilomita 2.5.Wakaazi wa kisiwa cha Tumbatu wamegawika katika sehemu kuu mbili. Nao ni wale Wanaoishi Jongowe ambao wako kusini ya kisiwa hicho na wale wanaoishi Gomani ambao wako kaskazini kwa kisiwa hicho. Wenyeji wa kisiwa hicho hujuilikana kwa jina la watumbatu.

Vilevile kisiwa cha Tumbatu kiko kaskazini “A” Unguja ambacho hivi sasa huitwa wilaya ndogo ya Tumbatu. Wazungumzajiwakubwa wa kitumbatu ni watumbatu wenyewe. Wakaazi wa kisiwa hiki wanakadiriwa kuwa ni watu 370,000 ambao hujishughulisha zaidi na uvuvi, biashara, kilimo, ufugaji nk.
Kwa upande wa lugha, lugha moja hutofautiana na lugha nyengine na ndipo hujitokeza lahaja. TUKI ( 2004 - 2005 ) amesema kuwa “ lahaja ni tofauti ya matamshi, maumbo na matumizi ya maneno mbalimbali kwa lugha yenye asili moja.”

## 1.2 Usuli waTatizo

Tafiti kuhusu lahaja za Kiswahili zilianza kujitokeza siku nyingi.Miongoni mwa kazi za mwanzo ni ile ya Stigand (1915) anayeleza kuwa lengo lake lilikuwa ni kusambaza maneno mengi ya lahaja kutokana na hofu kwamba mabadiliko makubwa yaliyokuwa yakitokea yangeweza kusababisha kupotea kwake. Hivyo kimsingi kazi yake ilijihusisha zaidi na orodha ya maneno ya lahaja kwa nia ya kuyahifadhi kimaandishi.Vilevile, Stigand (ameshatajwa) amebainisha lahaja 15 za Kiswahili ambazo kwa wakati huo bado ubainishaji wake haukufanyika kwa misingi ya kitaaluma.

Mbaabu (1991) aneleza changamoto zilizokuwepo mwishoni mwa karne ya 19 katika harakati ya kuichagua lahaja moja ya kuisanifisha. Pamoja na changamoto zilizokuwepo, mwisho, lahaja yaKiunguja Mjini ilisanifiwa.Jambo hilo lilisababisha kuibuka kwa lahaja ya Kiswahili sanifu iliyopewa hadhi ya kutumika katika sehemu za kazi, kwenye vyombo vya kutunga sheria, na maandishi yake kutawala kwenye vitabu kadhaa vya kitaaluma.Kamati na mabaraza mbalimbali yaliundwa kwa lengo lakukitetea Kiswahili Sanifu. (Maganga 1997) Kamati na mabaraza hayo yalifanya kazi yake na hatimaye kukubaliana kwamba lahaja ya Kiunguja Mjini ndio isanifishwe na kuwa Kiswahili Sanifu. Hata hivyo ni jambo lisilopingika kwamba, wengi kati ya wanakamati hao walikuwa ni Wazungumzaji ambao hakuwa na ujuzi wa kutosha katika taaluma ya lugha hususani lugha ya Kiswahili na lahaja zake.Kutokana na ukweli huu kulikuwa na makosa mengi katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili uliofanywa na watu hao (Maganga 1997). Pamoja na makosa hayo, kuwepo Kiswahili Sanifu kilichofanywa na watu hao ndicho

kilichokubalika na serikali na kutumika katika shughuli rasmi kama vile elimu,utawala, mahakama na katika mikutano ya hadhara.

Mbaabu (2003) anaeleza kwamba, lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kiasi kwamba zile zinazofahamika kwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili ni chache tu kutokana na kutozitafiti vya kutosha. Anaendelea kueleza kwamba, jambo lililowafanya wataalamu hao wa Kiswahili kutoitafiti lugha hii kwa upana unaostahiki ni dhana kwamba Kiswahili Sanifu ndiyo hasa Kiswahili chenyewe na hivyo kupuuza lahaja mbalimbali. Masebo na Nyangwine (2006,2007, 2008) katika ufafanuzi wao juu ya maana ya lahaja katika lugha ya Kiswahili pamoja na mambo mengine wanakiri kwamba kuna tofauti mbalimbali zinazojitokeza kutoka lahaja moja na nyingine.

Miongoni mwa mambo yanayotofautisha lahaja hizo ni lafudhi, fonolojia na msamiati.Maelezo haya yanatoa ufahamu kwamba kama kuna tofauti za kifononolojia, msamiati na lafudhikati ya lahaja moja na nyingine ni wazi kwamba kuathiriana kwa lahaja hizo katika vipengele hivyo ni jambo lisilopingika.Tunasema hivi kwa sababu jamii ya Watumbatu kwa mfano, huzungumza Kitumbatu katika shughuli na mawasiliano katika sehemu kubwa ya maisha yao ya kila siku.Kwa msingi huu,wanapokuwa katika shughuli rasmi ambapo wanalazimika kuzungumza Kiswahili Sanifu ni wazi kwamba athari za lahaja ya Kitumbatu zimejitokeza katika Kiswahili Sanifu bila hata ya wao kutarajia. Msanjila (2006) anaeleza kwamba ni vigumu sana kuitenganisha jamii na lugha yake kwa kuwa lugha na jamii ni kama pande mbili za sarafu moja.

Kitala (2006) anaeleza kwamba, utamaduni uliopo ndani ya lugha ya Kiswahili hubainika katika lahaja zake. Anaendelea kueleza kwamba ukitaka kuufahamu vizuri utamaduni wa lugha ya Kiswahili basi pitia lahaja zake mbalimbali ndipo utaona utajiri wa utamaduni upatikanao katika ugha ya Kiswahili. Suala kwamba katika lugha kumesheheni utamaduni wa jamii husika ni jambo lisilopingika kwa namna yoyote ile kwa kuwa ni jambo la kweli ambalo limethibitishwa na tafiti mbalimbali ambazo zimeshafanyika.Maelezo haya yanasisitiza uelewa wetu kwamba Kama katika ama lahaja nyingine tofauti na ile ya kweli. Kitumbatukina utamaduni wake kama zilivyo lugha ama lahaja nyengine za lugha ya Kiswahili jambo ambalo linafanya mzungumzaji wa Kitumbatu kudhihirishautamaduni huo pale anapozungumza KiswahiliSanifu.Katika kudhihirisha utamadunihuo ndipoathari za Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu huonekana.

Hivyo basi wanafunzi na walimu wao wanapokuwa shuleni husisitizwa kutumia Kiswahili Sanifu katika mawasiliano mbalimbali baina yao. Hata hivyo pamoja na msisitizo huo bado hujitokeza athari mbali mbali zikiwemo za kiisimu na lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika shuleni. Kwa msingi huo basi, utafiti huu umefanywa ili kuchunguza *‘athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar.”*

### 1.3 Tatizo la Utafiti

Kutokana na kukua na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili Sanifu katika mazingira rasmi, kumekuwa na mijadala mingi kuhusu athari ya lugha hii kwa lugha nyingine za kijamii (taz. K.m. Mochiwa, 1979).Pia imewahi kuchunguzwa jinsi lugha hizi za kijamii zinavyoathiri matumizi ya Kiswahili hasa katika mazungumzo pale matamshi

ya lugha ya kijamii yanapojitokeza katikaKiswahili Sanifu. Hata hivyo, mijadala kama hii haijawahi kuhusisha lahaja za Kiswahili ambazo nazo ni lugha za kijamii na zenye uhusiano na lahaja na vile vile uwezekano wa kuathiri lahaja sanifu.

Kwa kuwa hakuna tafiti zilizofanyika kuhusu athari za lahaja mbalimbalikatika mazingira yaliyo rasmi ndipo mtafiti alipoamua kufanya utafiti ili kuchunguza "*Athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katikaKiswahili Sanifu kinachotumika katika shule Tumbatu Zanzibar."*

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni haya yafuatayo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu nikuchunguza *"athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar".*

### 1.4.2 MalengoMahususi

(i) Kuchunguza mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia inayotokana na lugha ya Kitumbatu iliyoathiri Kiswahili Sanifu.

(ii) Kufafanua athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu.

(iii) Kuchunguzasababu zilizosababisha athari hizo katika Kiswahili Sanifu.

## 1.5 Maswaliya Utafiti

(i) Ni mifanyiko ipi ya Kifonolojia na Kimofolojia inayotokana na lugha ya Kitumbatu iliyoathiri Kiswahili Sanifu?

(ii) Kuna athari gani za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika Shule za Tumbatu Zanzibar?

(iii) Ni sababu gani zilizosababisha athari hizo katika Kiswahili Sanifu?

### 1.6 Umuhimu waUtafiti

Utafiti huu utawasaidia walimu na wanafunzi kuelewa athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar. Pia, utawasaidia kufahamu sababu za athari za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu za Zanzibar ili kuziepuka.Vilevile utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika nadharia ya Isimu.

### 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia inayotokana na lugha ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu, kufafanua athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar pamoja na kuchunguza sababu zilizosababisha athari hizo katika Kiswahili Sanifu. Mtafiti ameangalia athari hizo katika kipengele cha matamshi, maumbo ya maneno na tungo tu. Mtafiti hakutembelea katika eneo lote la Tumbatu bali alifanya utafiti wake katika shule za Jongowe na Tumbatu tu.

### 1.8 Maadili ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maadili nakanuni za kufanya utafiti. Mtafiti ameomba kibali kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na katika taasisi zinazohusika ili kupata ridhaa ya kukusanya data katika maeneo teule, pia amewaomba

watafitiwa ridhaa ya ushiriki wao na kuahidi kutunza siri zao. Jambo lolote linalokwenda kinyume cha maadili ya utafiti halikufanywa na mtafiti.

### 1.9 Hitimisho

Sura hii ya Utangulizi imejadili Utangulizi wa jumla , Usuli wa tatizo, Tatizo la Utafiti. Malengo ya Utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, maadili ya utafiti na hitimisho.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YAKAZITANGULIZINA MKABALA WA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni maandiko yanayohusiana na mada husika ambayo tayari yameshaandikwa na watafiti wa kazi zilizotangulia. Mapitio hayo ni muhimu kwa matafiti ili kumwezesha kuelewa utafiti uliofanyika katika mada husikaa, pia humsidia kuelewa mbinu mbalimbali zilizotumiwa na watafiti waliotangulia. Vilevile husaidia katika kuepuka kutorudia kilichoandikwa. Sura hii imejadili maandiko kuhusu Kiswahili Sanifu, tafiti zinazozungumzia atahari za lahaja katika Kiswahili, kazi tangulizi kuhusu Kitumbatu, pengo la utafiti na Mkabala wa Nadharia.

## 2.2 Maandiko kuhusu Kiswahili Sanifu

Kiswahili Sanifu ni Kiswahili kilichofanyiwa marekebisho kutoka lugha nyengine na kuingizwa kwenye lugha husika. Usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ulianza mwaka 1930 ilipoundwa kamati ya lugha ya Afrika Mashariki. Suala la msingi ilikuwa ni kuteua lahaja mojawapo yalahaja za Kiswahili zisizopungua kumi na tano. Kamati hii iliamua kuisanifu lahaja ya Kiunguja mjini ambapo ilikuwa imeenea katika sehemu kubwa ya maeneo ya Bara hadi kufikia Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na nchini Burundi.

Kiswahili sanifu ni lugha isiyokuwa na makosa ya kisarufi. Hivyo, lugha hii huwa na sheria, kanuni, au taratibu zinazopaswa kufuatwa katika lugha fulani. Kila lugha huwa na kanuni zake lakini kwa upande wa Kiswahili Sanifu huwa tunazingatia kanuni za kisarufi kama vile sauti (utamkaji), aina za maneno, upatanisho wa

maneno kisarufi, muundo wa sentensi za Kiswahili na kadhalika. Kiswahili Sanifu hutumika kwamawasiliano baina ya wasemaji wa lahaja tofauti za lugha moja, pia hutumika katika shughuli rasmi.

## 2.3 Tafiti Zinazozungumzia Athari za Lahaja katika Kiswahili

Massamba na wenzake (2009) wameeleza historia fupi ya Kiswahili pamojana kuonesha lahaja za Kiswahili.Katika maelezo yao wamesemakuwa, yapo mambo ya kimsingi yenye kutofautisha lahaja moja na nyengine. Miongonimwa mambo hayo ni matamshi, msamiati, muundo na wakati mwingine maana ya maneno.Maelezo haya yanafanana na yale yaMuhura(2009) ambaye ameorodhesha ya lahaja 18 za Kiswahili na amesema kuwa miongoni mwa mambo yenye kupelekea lugha moja kuwa na lahaja tofauti ni umbali wa kijiografia, hamahama ya watu elimu na uhaba wa mawasiliano kati ya jamii moja na nyengine.

Mohamed (1984) alifanya utafiti unaohusiana na lahaja za Kipemba, Kiunguja Mjini pamoja na KiswahiliSanifu.Utafiti wake ukijihusisha zaidi na kueleza matamshi ya lahaja ya Kipemba, pamoja na kuzungumzia jinsi ukanushi unavyojitokeza ndani ya lugha hizo. Katika uchambuzi wake, amedhihirisha mambo mawili makubwa. Kwanza,misamiati kadhaa ya lahaja ya Kipemba na jinsi inavyotofautiana na Kiswahili Sanifu, pia ameonesha mabadiliko ya sauti mbali mbali na jinsi zinavyotofautiana kutoka maeneo ya mjini hadi vijijini. Aidha, ameonesha umilikishaji wa lahaja ya Kipemba ambao kwa kiasi kikubwa hutokea ndani ya nomino husika kama: nyumbayo’ badala ya nyumba yako, pahalape’ badala ya pahala pake, na ‘kisungwa’ badala ya kisu cha watu. Ni dhahiri kuwa vipengele

hivyo vya lahaja ya Kipemba vimemsaidia mtafitikupata mwongozo wa mambo ya kufanyia kazi wakati wa utafiti wake hususani wakati wa kuchunguza mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia inayotokana na lugha ya Kitumbatu iliyoathiri Kiswahili Sanifu.

Mbaabu (1991) aliandika kitabu kinachohusu historia ya Kiswahili na usanifishaji wake. Katika kuielezea historia hiyo anaeleza kuwa ingawa kulikuwa na lahaja nyingi, lakini lahaja ya kimvita na kiunguja ndio zilizokuwa katika ushindani mkubwa katika mchakato wa kuteua lahaja moja ambayo ndio itakuwa msingi wa Kiswahili Sanifu.Kazi ya Mbaabu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa itamsaidia mtafiti kufahamu historia ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake ambayo iliweza kutoa nuru kwa utafiti huu.

Maganga (1991) katikatasnifu yake ya Uzamivu amezizungumzia lahaja tatu za Zanzibar. Lahaja hizo ni Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu na kuzihusisha na Kiswahili Sanifu. Dhamira kuu ya kazi yake ni kuchunguza mofofonolojia ya lahaja za Kipemba, Kitumbatu naKimakunduchi huku akizihusisha na Kiswahili Sanifu. Kazihii ni muhimu kwa utafiti huu kwasababu itamsaidia mtafiti kupata baadhi ya misamiati ya Kitumbatu, pia kupata mwongozo wa uchambuzi wa data zake.

Maganga (1997) aliongelea pia suala la lahaja.Alizitaja lahaja mbalimbali za Kusini na Kaskazini, na kueleza jinsi lahaja zinavyotofautiana kati yao. Katika kielelezo cha lahajamama ya kusini, amekionesha Kimakunduchi na hivyo, itamwezesha mtafiti kuelewa asili ya lahaja aliyoifanyia utafiti..Whitely (1956) alifanyautafiti

kuhusu lahaja ya Ki- mtang'ata. Katika kazi yake ameelezea zaidi juuya matamshi ya lahaja hiyo. Jambo muhimu aliloligusiani kwamba lahaja zina sifa zake zenye kutofautiana baina ya lahaja moja na nyengine. Pamoja na hayo yapo baadhiya mambo yaliyo mahususi katika kila lahaja, kama vile mashina ya maneno.Kazi hii imemsaidia mtafiti kupata mwelekezo wa kuzielewa sifaza lahaja ambazo zimemwongoza katika kuzielewa sifa za kiisimu za lahaja iliyotafitiwa na hivyo kuwa rahisi katika kuainisha athari za lahaja tafitiwa katika Kiswahili Sanifu.

Masebo na Nyangwine (2008) wameendelea kuzungumzia lahajaya Kiswahili.Wamesema kuwa "Lahaja ni mojawapo ya lugha ambazo kusema kweli huhesabika kama lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele kama vile lafudhi, fonolojia(matamshi)msamiati isiokuwa msingi au miundo".Aidha wameziorodhesha aina mbalimbali za lahaja na kuainisha eneo inamopatikana kila lahaja.

Mwansoko, (2008) katika makala yake ameelezea juu ya umuhimu wakuzidi kuzifanyia utafiti lahaja za Kiswahili.Amesema kuwa katika kukieleze na kukiimarisha Kiswahili Sanifu ni muhimukuzitafiti lahaja ili ziweze kujazamapengo ya misamiati na kiistilahi. Maelezo ya makala hii yatatusukumana kututia hamu ya kufanya utafiti wa kina kuchunguza *athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika* Kiswahili Sanifu kinachotumika katika Shule za Tumbatu Zanzibar.

### 2.4 Kazi Tangulizi Kuhusu Kitumbatu

Kipacha (2003) katika kazi yake amejaribu kuonesha matini za Kitumbatu zikiwemo mashairi na hadithi.Vilevile ameonesha orodha ya leksimu za Kitumbatu zinavyotofautina na zile za Kiswahili Sanifu (kipacha 2003; 145 ) kama ifuatayo:

| **Kitumbatu** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) Kiza | giza |
| b) Gino | jino |
| c) Pakusa | pangusa |
| d) gani | jani |

Katika mifano hii tunaona kuwa sauti [g] katika Kitumbatuhubadilika na kuwa [ dʒ] katika Kiswahili Sanifu.Pia Kipacha ameeleza kwa ufupi sifa bainifu za kifonolojiaambapo amesema kuwa fonimu za Kitumbatu hazitofautiani na zile zaKiunguja.Vilevile ameonesha sifa nyengine za kifonolojia yaKitumbatu kuwana tabia ya udondoshaji wa nazali inayotangulia vikwamizi, mfano katika maneno kama kazu (kanzu), aza (anza), katika maneno haya tunaona kuwa nazali - n - inadondoshwaambapo hali hii inaonesha maumbo ya Kitumbatu yaliyotafauti na Kiswahili. Pia amezungumzia masuala ya kimofolojia,kama vile suala la mofimukanushi ambayo katika Kitumbatu ni he:

Kamakatika neno he – twekwenda hatukwenda, he- twecheza hatukucheza, he – twesoma hatukusoma.Ingawa amejaribu kutoa kwa uchache baadhi ya sifa za kiisimu za kibantu, lakini baadhi ya taarifa hizo zinaonesha hali tofauti na vile ilivyo hasa katika Kitumbatu. Kwa mfano ameeleza kuwa umbo - vu – kama lilivyo katika neno kevu ni sawa na kitenzi “kuwa”katika Kiswahili Sanifu.Lakini neno hilo ni kavu linapotumika kwa nafsi ya tatu umoja maana yake ni ‘ alikuwa’ kama ilivyokuwa kwa waandishi wengine.

Stude (1995) ni mtaalamu mwingine aliyenukuliwa na Kijakazi (2012) ambaye alifanya utafiti katika lahaja ya Kitumbatu kwa kuangalia urekebishaji na mabadiliko ya lugha katika Kitumbatu. Aliangalia tofauti za sauti kati ya Kitumbatu na Kiswahili Sanifu na kueleza kuwa Kitumbatukina sauti [1*] inayotamkwa pamoja na irabu inayofuatana nayo na kuipa sauti hii sifa ya vokali.Sauti hii haipatikani katika Kiswahili Sanifu.Pia ameonesha mabadiliko ya sautina tofauti ya msamiati katika Kitumbatu na Kiswahili Sanifu na aliingiza baadhi ya mifano kutoka katikalahaja ya Kimakunduchi. Kwa mfano sauti [I] inayokaa mwanzoni mwa neno katika Kitumbatu hujitokeza kama /j/ katika Kimakunduchi na hujitokeza kama / u / katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Lakini [v]kama vumbi kwenye Kiswahili Sanifu huwa [d] katika Kitumbatu,neno "lala"hutofautika kimatamshi kwani Kitumbatu hutumia / I* / yenye uvokali na hutamkwa /I*aI*a/.Sauti [ y] au fonimu /j/ huoneshwa pia katika Kimatamshi.

Tuangalie mifano hii kama ifuatayo:-

| **Kitumbatu** | **kimakunduchi** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| L*umia | Yumia | Umia |
| L*umiza | Yumiza | Umiza |
| L*omba | Yomba | Omba |
| L*al*a | Yaya | Lala |

Mifano hii huonesha maneno yanayoanza na sauti [I] katika Kitumbatu yanaanzana irabu katika Kiswahili Sanifu..

Bakiza (2012) wao pamoja na kutoa maana za maneno kwa lahaja ya Kitumbatu pia wametoa tafauti ya sarufi ya Kitumbatu na sarufi ya Kiswahili. Sarufi yalahaja ya Kitumbatuinafanana na sarufi ya Kiswahili Sanifu, ingawa matamshi yanayotofautiana.

Mfano katika viwakilishi vya nafsi kamaifuatavyo:-

| **Nafsi** | **Kiswahili Sanifu** | **Kitumbatu** |
|---|---|---|
| Nafsi ya 1 umoj | Mimi ninakuja | Miye sakuja |
| Nafsi ya 1 wingi | Sisi tutakuja | suye tuchakuja |
| Nafsi ya 2 umoja | Wewe utakuja | weye kuchakuja |
| Nafsi ya 2 wingi | Nyinyi mtakuja | nyuye muchakuja |
| Nafsi ya 3 umoja | Yeye atakuja | veye kachakuja |
| Nafsi ya 3 wingi | Wao watakuja | veo wachakuja |

Stigand (1915) akinukuliwa na Kijakazi (2012) ameandika kuhusu mabadiliko ya kisarufi katika lahaja za Kiswahili akidai kuwa lahaja hizo zimegawika katika makundi kumi na tano.Makundi hayo anyataja kuwa ni kundi la Zanzibar lenyelahaja kuu za Kiunguja, Kimrima na Kimgao, lahaja ndogo za Zanzibar ni Kitumbatu, Kihadimu na Kipemba. Katika kazi yake hii ameeleza mabadiliko katika lahaja ya Kimvita, Kimgao naKiunguja. Mabadiliko aliyoyaonesha ni pamoja na mabadiliko ya sauti, mabadiliko ya sarufi, mabadiliko ya msamiati na mabadiliko ya nahau. Kwa mfano, kuhusu mabadiliko katika sauti baina ya Kiunguja na Kimvita,

anaeleza kuwa [ch] au fonimu / ʃ / katika Kiunguja huwa sauti [t] au fonimu / t / katika Kimvita na sauti [ j]au fonimu / *ƒ* / katika Kiunguja huwa sauti [d] au fonimu / d/ katika kimvita, kama katika mifano ifuatayo : -

| | |
|---|---|
| a [ tʃ ] Kiunguja | [t] Kimvita |
| mchanga | mtanga |
| macho | mato |
| b) [ *ƒ* ] njaa | [t] ndaa |
| nje | nde |

Mifano hii katika (1) imetuonesha mabadilikoya sauti katika lahaja ya Kiunguja naKimvita lakini hakutueleza mabadiliko yoyote ya lahaja yaliyomo katika Kitumbatu. Ameeleza tu kuwa Kitumbatu ni lahaja inayopatikana Kaskazini mwa kisiwa cha Zanzibar Unguja nakuwa Kihadimu ni lahaja ya Mashariki na Kusini ya kisiwa cha Zanzibar.

Kijakazi akimnukuu Hill (1973) amesemakuwa alifanya utafiti katika Kitumbatu na

Kimakunduchi kwa kuangalia sauti zilizomo ndani ya lahaja hizo.Aliangalia sauti [o], [t], [c], na [k] ili kuona msambao wa sauti hizo katika lahaja nyengine tisa kamaChifundi, Kiamu, Kijomvi, Kimiini,Kimtangata,Kimvita, Kipemba, Kiunguja, Kisiu na Kitikuu.

Maganga (1991) vilevile akinukuliwa na Kijakazi (2012) alisema kuwa alifanya utafiti juu ya mofofonolojiakatikalahaja za Kiswahili akilinganisha maumbo hayo katika lahajaza Kitumbatu, Kipemba, Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu. Katika

utafiti huu lahaja ya Kitumbatu ililinganishwa na lahaja nyingine katika kipengele cha mofofonolojia ambapo masuala kama ya tangamano la irabu yaliangaliwa hadi katika ngazi ya aina za maneno kama vile nomino, vitenzi na kadhalika. Katika Kitumbatu alionesha tangamano la irabulinavyotokea. Kwa mfano, wakati viambishi vya nafsi vinapokutana na mzizi wa kitenzi unaoanza na irabu, matokeo huwa kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

| **Kitumbatu** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| A ) nyambile (ni + ambile) | niambie |
| B ) weze (u + eze) | utafute |
| c ) etwe (a+ itwe) | aitwe |
| d) ende (a + ende) | aende |
| e) tone ( tu + one) | tuone |

Mifano hiyo imeonesha kuwa irabu katika viambishi nafsi hubadilika kwa namna mbalimbali au kudondoshwakabisa.Utafiti huu ni muhimu sana kwani utatusaidia kupata *athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswhili sanifu.*

Nurse na Hinnebush (1993) wameeleza kuwepo kwa uhusiano wa msamiati katika lahaja za Kiunguja mjini.Walifafanua kwa kusema kuwa msamiati wa lahaja za Kitumbatu na Kimakunduchi ambacho ni lahaja za asili ya kusini na ina sifa zifuatazo:-

a) huingiza au kudondosha sauti /l / au / y / kwa mfano:-

i. _lawa / _ yawa _ ondoka

ii. - laga / - aga

iii. -Lola / yoya - tazama

iv. -Vy aya / - vyaa - zaa

v. -Ula / - uya - ua

vi. –mguyu - mguu

b) Hazina sauti / v/ katika maneno yake. Kwa mfano:-

i. – udi rudi

ii. – afiki rafiki

c. Hudondosha nazali zinapokuwa:

i. kabla ya vikwazo ghuna kwa mfano:-

aza -- anza

ii. katika nomino za silabi moja katika ngeli ya 9 / 10 kwa mfano:

a. Cha - ncha

b. Chi - Nchi

iii. Kabla ya kipasuo ghuna. Kwa mfano

Fungua -Fungua

Maelezo hayo yamemshawishi mtafiti na kuamua kufanya utafiti wa kina katika kuchunguza *athari za kiisimu za lahajaya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar.*

## 2.5 Pengola Utafiti

Kwaujumla, lahaja ya Kitumbatu ni miongoni mwa lahaja zilizofanyiwa utafiti katika maeneo tofauti lakini tafiti hizo hazikutosheleza kwani kuna maeneo

mengiyanayohitaji kufanyiwa utafiti. Kutokana na kuwa hakuna andiko lolote linalohusu athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar ndipo mtafiti alipoamua kuziba pengo hili kwakuchunguza "*athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar"*

## 2.6 Mkabala wa Nadharia

Kwa mujibu waMassamba na wenzake (2009) Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi iliyojengwa kwa pamoja kuikamilisha kwa madhumuni ya kuwa kigezo cha kuelezea jambo au mambo kadhaa.

***Nadharia Kidhi ya Mawasiliano ( NKM ) .***

Utafiti huu umeongozwa na *Nadharia Kidhi ya Mawasiliano*( NKM). Hii ni nadharia ya mawasiliano iliyoanzishwa na Howard Giles (1973) ambayo hapo awali ilijulikana kwa jina la "Speech Accomodation Theory".

Giles alianzisha nadharia hii katika kujaribu kutafuta sababu za kuwepo kwa mabadiliko ambayo aliyaona katika matamshi ya watu wengi wakati wanapozungumza na watu wengine na hivyo kutaka kujua matokeo ya tabia hiyo. Hivyo, lengo kuu la nadharia hii ni kueleza sababu za kubadili mtindo wa matamshi wakati wa mawasiliano ya kijamii na kuangalia athari zake katika jamii.

Nadharia Kidhi ya Mawasiliano inasema kuwa "binaadamu hujitahidi kuzungumza lugha au kuiga namna fulani ya matamshi ya lugha ya msikilizaji wake ili aweze kukidhi haja ya mawasiliano." Hufanya hivyo kwa kujua au bila kujua, kwa kufikiria

au bila ya kufikiria na huiga msamiati au vipengele vyengine vya lugha kwa mtu anayezungumza naye.

Nadharia hii inazidi kufafanua kuwa mkutano au mawasiliano ya kiisimu yanafasiliwa kama mbinu, ambapo watu huiga tabia ya kimawasiliano inayotumiwa na watu wengine kwa lengo la kukubalika katika jamii hiyo. Kwa mfano mzungumzaji “A” huweza kuiga mtindo fulani kwa matamshi ya lugha kwa ajili ya mzungumzaji “B” ili kukidhi lafudhi ya lugha husika ya lugha inayoigwa kwa lengo la kukidhi au kutimiza malengo yake. Giles anafafanua kuwa sababu kuu ya kubadili mtindo wa matamshi ni kuonesha makubaliano na uhusiano kwa watu wengine hali hii huwafanya watu wengine kujihisi kuwa wanahusiana.

Kwa mujibu wa nadharia hii, mawasiliano au makutano ya kiisimu yamegawika katika madaraja mawili ambayo ni mawasiliano au makutano wima na yasiyowima. Mawasiliano au makutano wima ya kiisimu hutokea pale mtu anapozungumza na mjuzi wa lugha na akajizalimisha kuzungumza lugha yake ili aweze kumfikia. Mawasiano au makutano yasiyowima hutokeya pale mtu anapozungumza na watu kama vijana na akajilazimisha kurahisisha lugha ili kukidhi haja ya mawasiliano. Hivyo, nadharia hii inatilia mkazo lugha, muktadha na utambulisho.

Nadharia Kidhi ya ya Mawasiliano (NKM) inaona kuwa:

(i) Watu hueleza historiana uzoefu wao katika mawasiliano kupitia matamshi na tabia zao ili kuonesha kuwepo kwa ufanano wa matamshi na tabia fulani katika mazungumzo.

(ii) Mawasiano huathiriwa na namna watu wanavyopokea na kutathmini nini kimetokea katika mazungumzo, yaani namna gani watu wanatafsiriwa kuhukumu ujumbe uliobadilishwa katika mazungumzo.

(iii) Mawasiliano hubadilika kulingana na kaida na hali ya kimuktadha inayofaa.

Mtafiti ameamua kutumia nadharia hii kwa sababu ina uwezo wa kutumiwa katika maeneo yoyote ambayo yanahusisha mawasiliano katika lugha ya mazungumzo.hivyo inatoa mwongozo unaofaa.

Vile vile kwa kuwa lengo kuu la nadharia hii ni kuchunguza *athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar*, mtafiti aliona umuhimu wa kutumia nadharia hii ( NKM ) kwa sababu inaendana na utafiti huu ambaoumechunguza sababu mbalimbali zilizosababisha athari za Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu wakati wa mazungumzo.

## 2.7 Hitimisho

Sehemu hii imezungumzia mapitio ya kazi tangulizi naMkabala wa Nadharia. Sura imeanza na utangulizi, maandiko kuhusu Kiswahili Sanifu, tafiti zinazohusu athari za lahaja katika Kiswahili, kazi tangulizi kuhusu Kitumbatu, pengo la utafiti na imemalizia na mkabala wa nadharia.

# SURA YATATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imezungumzia mbinumbalimbali ambazo mtafiti atazitumia katika kutekeleza kazi yake.Vilevile sehemu hii imebainisha, kubainisha eneo la utafiti, kundi lengwa la utafiti, uteuzi wa sampuli, jinsi data zilivyokusanywa, vifaa vitvyotumika wakati wa kazi yenyewe, na mwisho sura imeeleza jinsi uchambuzi wa data ulivyofanyika.

## 3.2 Eneo laUtafiti

**Uta**fiti huu utafanyika katika Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja, katika Skuli nne zilizomo Kisiwani Tumbatu ambazo ni Shule za msingi Jongowe, Shule ya Sekondari Jongowe, Shule ya msingi Tumbatu na Shule ya Sekondari Tumbatu.Mtafiti amekusudia kufanya utafiti wake katika eneo hilo kwa sababu ndio sehemu ambayo watafitiwa wanapatikana kwa urahisi na kwa muda mfupi , pia ndio watakaotoa data sahihi.

## 3.3 Kundi Lengwa

Walliman (2011) amefafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwautafiti (vinavyotafitiwa) yaani watu, taasisi, vitu au matukio kwa ujumla. Vilevilekundi lengwani jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli ya utafiti inaweza kuchaguliwa. Katika utafiti huu kundi lengwa ni walimu na wanafunzi wa somo la Kiswahili katika shule ya msingi Jongowe na Tumbatu pia walimu wa Shule ya Sekondari Jongowe na Tumbatu. Mtafiti ameamua

kuchagua walengwa hao kwa sababu ndio wenye uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika katika utafiti huu.

### 3.4 Sampuli naUsampulishaji

#### 3.4.1 Sampuli.

Kothari (2004) anafafanua sampuli kuwa ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo mtafiti humpatia data na kutoa mahitimisho yake. Utafiti huu unahusisha sampuli ya watu**68**.Miongoni mwaowalimu**29** wa Shule za msingi na Sekondari za Jongowe na Tumbatu ambao wanaofundisha somo la Kiswahili na wanafunzi**39**wa Shule za msingi na Sekondari zaJongowe na Tumbatu wanaojifunza somo la Kiswahili. Mgawanyo wa sampuli utawasilishwa kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na 3.1: idadi ya Sampuli ya Watafitiwa**

| **Shule** | **Shule ya Sekondari Jongowe** | | **Shule ya Sekondari Tumbatu** | | **Shule ya Msingi Jongowe** | | **Shule ya Msingi Tumbatu** | | **Jumla Kuu** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| WATAFITIWA | W/K | W/M | W/K | W/M | W/K | W/M | W/K | W/M | W/K | W/M | JUMLA |
| WALIMU | 02 | 04 | 08 | 03 | 05 | 02 | 01 | 04 | 16 | 13 | **29** |
| WANAFUNZI | 05 | 05 | 06 | 06 | 05 | 04 | 04 | 04 | 18 | 21 | **39** |

#### 3.4.2 Mchakato waUsamplishaji

Kwa mujibu wa Sigh (2007) usamplishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Sampuli huchaguliwa kwa njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na usamplishaji nasibu na isiyo nasibu (usamplishaji usionasibu).Ruane (2005) anafafanua usamlishaji nasibu kuwa ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua memba yeyote katika kundi lengwa huwa mkubwa. Kwa maneno

mengine,usamplishaji nasibu ni mbinu ya kuchagua sampuli ambapo kila memba katika kundi lengwa ana fursa sawa ya kuchaguliwa kuingia katika utafiti. Usamplishaji usio nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambao hutegemea zaidi maamuzi ya mtafiti na hauwezi kutoa matokeo jumuishi kuhusiana na kundi lengwa. Yaani,ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo sehemu ya watafitiwa kuchaguliwa kwa kuzingatia zaidi upatikanaji wao kuliko uwakilishi wao. Moja kati ya sampuli inayopatikana kwa njia hii ni sampuli ya makusudi. Sampuli ya makusudini aina ya sampuli ambayo mtafiti huchagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa Kwa hivyo utafiti huu umetumia sampuli ya makusudi iliyochaguliwa kwa njia ya usamplishaji usio nasibu kwa sababu kundi hilo ndilo lenye uwezo wa kutoa taarifa sahihi.

### 3.5 Mbinu za Utafiti

**Kothari** (2004) anafafanua kuwa, mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti.Mbinu za utafiti ziko katika makundi makubwa mawili, ambayo ni mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchanganua data.Mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti. Utafiti huu umetumia data ya upili namsingi kama ifuatavyo:

#### 3.5.1 Data ya Upili

Data ya upili ni aina ya data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma ambazo hukusanywa kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti (Kothari 2008). Madhumuni hasa ya kukusanya data hizi ni kujaliza data za msingi ili kusaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Data hizi zimekusanywa kutoka katika vitabu, makala, majarida, tasinifu, tovuti na wavuti.

Ili kuweza kuzipata data hizi, mtafiti amelazimika kwenda maktaba mbalimbali kutafuta maandiko yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa kina. Miongoni mwa maktaba alizozitembelea ni pamoja na Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar,maktaba Kuu ya Zanzibar na maktaba ya Bakiza.

### 3.5.2 Data zaMsingi

Data za msingi kwa kawaida huwa data ghafi ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya kujibu maswali yake ya utafiti na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingineyeyote kwa minajili ya utafiti kama huu unaofanywahivi sasa (Kothari 2008). Data hizi zilikusanywa madarasani kutoka kwa watafitiwa mbalimbali walioteuliwa na mtafiti na ambao anatambua kwamba watampatia data muafaka zitakazosaidia kujibu maswali yake ya utafiti. Data hizi pia hukusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazoni usaili, hojaji nauchunguzi shirikishi.

#### 3.5.2.1 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa wasailiwa.Maswali hayo yamejibiwa kwa njia ya mdomo na kuandikwa kwenye daftari la kumbukumbu.Kwa mujibu wa Kothari (1990) mbinu hii inaruhusu utoaji wa ufafanuzi pale inapoonekana taarifa fulani haijaeleweka vyema wakati wa kuuliza maswali.Mbinu hii husaidia kuweka wazi istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watu wanaoulizwa maswali. Pia itasaidia kupata taarifa za ziada na kina zaidi; hususani pale ambapo majibu ya watu wanosailiwa yanapokuwa hayaeleweki.Vilevile usaili umemsaidia mtafiti kugundua mahusiano magumu

katika mahusiano ya kijamii na hivyo kumwezesha kuwa karibu na watoa habari.

**3.5.2.2 Mbinu ya Hojaji**

Hojaji kwamujibu wa Kothari (1990) ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti ameandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani.Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemeana na taarifa inayohitajika na mtu anayepewa hojaji hizo. Mbinu hiihutoa fursa kwa mtafiti kuwaachia watafitiwa hojajiili wajaze kwa muda wao halafu huzikusanya baada ya muda waliokubaliana kufika. Fursa hii itamfanya mtafiti kupata muda wa kuendelea na shughuli zake nyimgine wakati watafitiwa wakiwa wamebaki na hojaji hizo wakizijaza.

**3.5.2.3 Mbinu ya Uchunguzishirikishi**

Mtafiti ameingia darasanina kuchunguza mawasiliano ya kiufundishaji na ya kimazungumzo ya wanafunzi na walimu kwa lengo la kupata data sahihi juu ya athari za kiisimu katika lahaja hiyo katika KiswahiliSanifu.Mtafiti ameingia darasani na kuona namna wanafunzi na walimu wanavyowasilianakwa kupata data sahihi kwa mujibuwa utafiti huu.Vile vile, mtafiti ametoka nje ya darasa wakati wa mapumziko na kuchunguza mawasiliano yao wakiwa nje ya darasa kwa lengo la kupata data sahihi.

## 3.6 Zana za Utafiti

Mtafiti ametumia zana kama vile kinasa sauti, daftari, na hojaji. Kinasa sauti kimemsaidia mtafiti katika kunasa sauti za watafitiwa wake kwaajili yakumbukumbu za baadayewakati wa uchambuzi wa data. Kwa upande wa daftari, kifaa hiki

kimetumika kwa kuandika baadhi ya taarifa muhimu zilizotolewa nawatafitiwa.Taarifa hizo zliandikwa kwa muhtasari, wenye kueleweka. Muhtasari huo ndio uliomwezesha mtafiti kujua namna ya kuanza uchambuzi wa data zake, na hatimaye, kuanza ripoti ya kazi nzima. Pia mtafiti aliandaa hojajizenye maswali kadhaa na kuwapatia watafitiwa ambao walizijaza na kutoa data zilizowezesha kuandikwa kwa tasnifu.

### 3.7 Hitimisho

Sura hii imeanza na utangulizi, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mchakato wa usampulishaji, mbinu za utafiti na mwisho sura imemalizia na zana za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kuwasilisha na kuchambua data zilizokusanywa juu ya mada ya " *Athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar".*

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo inawezesha kukamilisha malengo ya utafiti husika. Kothari (2008) anaeleza kwamba uchambuzi wa data ni hatua muhumu katika utafiti ambayo husaidia kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Hivyo basi, katika utafiti huu mbinu za uchambuzi wa data za kimaelezo na kimahesabu ndizo zilizotumika katika uchambuzi wa data.

Mbinu ya uchambuzi wa data ya kimaelezo inaelezwa kama mbinu isiyohusisha mahesabu bali ni maelezo ya kina tu ndiyo hutolewa katika kufafanua data ili kukamilisha malengo ya utafiti (Kothar). Mbinu ya uchambuzi wa kimahesabu ni ile inayohusisha tarakimu kama vile asilimia na idadi ya watafitiwa ama vitafitiwa.Mtafiti ametumia mbinu hii kwa kuchunguza na kuchambua idadi ya watafitiwa waliojibu maswali husika yaliyomo katika hojaji na kuyaweka katika asilimia kisha kuyafafanua kwa maelezo.

Mbinu zote hizi mbili zimetumika katika uchambuzi wadata za utafiti wetu. Mtafiti ameamua kutumia mbinu hii kwa sababu ndiyo inayokubaliana na utafiti

huu.Sura imeanza kwa kuwasilisha data na kumalizia na uchambuzi wa data. Uwasilshaji na uchambuzi huo wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti na maswali yanayoambatana na malengo hayo.

## 4.2 Mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia Inayotokana na LahajayaKitumbatu Iliyoathiri Kiswahili Sanifu

### 4.2.1 Sauti za Kitumbatu

Lahaja ya Kitumbatu ni lahaja ya Kiswahili yenye mfumo wa sauti za irabu na konsonanti. Mtafiti amechunguza aina hizo na kuonesha namna zilivyo katika lahaja ya Kitumbatu kama ifuatavyo:

### 4.2.2 Mfumo wa Irabu katika Kitumbatu

Irabu ni aina ya vitamkwa ambavyo hutolewa moja kwa moja pasi na kuwepo kizuizi chochote katika mkondohewa utokeao mapafuni ukipitia katika chemba ya kinywa au chemba ya pua (Massamba na wenzake, 2004; 24). Lahaja ya Kitumbatu ina irabu tano za msingi. Irabu hizo hujitokeza katika jozi bainifu kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

a) **/ i**/ : / pon**i** / “ kuku bo**i**” / pon **Ɔ** / “ aina ya samaki” : / g**i**na / “jina” / g**Ɔ**nd/ “fumania” : / kiko / k**i**ko “kifaa cha kuvutia tumbaku” / k**Ɔ** ko / “mikono”.

b) **/ ɛ**/ **:/ u**/ **:/ ɛ**za/“tafuta” / **u**za / “uliza” : / punj**ɛ** / “ chembe ya nafaka” punj**u** / “sumu ya kienyeji: / uj**ɛ**ya / “ kitoweo kinachotengenezwa kwa nyama ya taa au bunju” /uj**u**ya / “ gamba la nyoka”.

c) / Ɔ / : /**ɑ** / : / tojƆ / “tone” / toj**ɑ** / “dondoka” ; / mchag**ɑ** “mchelema” / mchag**Ɔ** / “sehemu ya kuekea kichwa kitandani wakati wa kulala” ; / I*Ɔ**I***a / “ oa, ona” / I*a / “lala”

Irabu hizi zinazojitokeza katika jedwali Na 2 lifuatalo:

**Jedwali Na. 4.1: Mfumo wa Irabu za Kitumbatu**

| | | |
|---|---|---|
| Mbele juu | I U u | Nyuma juu |
| | ɛe Ɔ | |
| Mbelekati | ɑ a | Nyuma kati |
| Chini | | |

Jedwali hilo linaonesha kuwa irabu **i** hutamkwa mbele ya chemba ya kinywa ulimi ukiwa umeinuliwa juu. Kwa hivyo irabu hii ni ya mbele juu. Irabu **ɛ**hutamkwambeleya chembaya kinywa ulimi ukiwa katikati na hivyo huwa ya mbele kati. Irabu nyengine ni**ɑ**ambayo hutamkwa chini ya chemba ya kinywa na hivyo huwa na sifa ya chini. Irabu **Ɔ** hutamkwa nyuma kati, ulimi ukiwa katika ulalo wa kati na hivyo huitwa irabu ya nyuma kati. Irabu **u** hutamkwa nyuma juu, ulimi ukiwa umeinuliwa juu kwa kiasi na hivyo hupewa sifa ya nyuma juu.

Pia, irabu katika Kitumbatu zinaweza kuwafinye au wazi. Irabu finye ni irabu ambazo zinatamkwa kwa kuwekwa upenyu mfinyu katika kinywa na ulimi ukiwa umeinukiwa ama kwa mbele au kwa nyuma (TUKI) na irabu wazi ni zile ambazo zikitamkwa ulimi unakuwa chini katika kinywa na midomo huwa wazi. Irabu hizo zinajitokeza katika Kitumbatu kama inavyoonekana katika mchoro **1** uliotangulia hapo juu. Pia inaonekana katika mifano ifuatayo ya jozi bainifu:-

(a) **/ a**/ :/**ɑ** / : / chw**a**ka / “jina la kijiji” / ch**ɑ**ka / “msituuliojifunga” / chw**a**go / “aina ya kaa” / ch**ɑ**go / “sehemu za kuwekea kichwa wakati wa kulala kitandani”

(b) /**e**/:/**ɛ**/: /bw**e**ka/ “kemeza” /b**ɛ**ka/ “tamko la kuitika” /ndw**e**le / “balaa, maradhi” /nd**ɛ**we/ “sehemu ya chini ya sikio”.

(c) /**u**/; /**u**/: / fy**u**fy**u /** “dhuluma” /f**u**f**u**/ “tipitipi” / ky**u**no/ “kiuno” /k**u**no / “ huku”; / fy**u**sa / “rusha”/f**u**sa/ “viza”.

Mifano hiyo inaonesha irabu finye zilizomo katika herufi mkozo wa irabu wazi zikiwa mbele yake. Irabu **/ i/**na /**Ɔ** / hazikujitokeza hapo kama irabu finye lakini zinaonekana kuwa ni irabu wazi kama inavyoonekana katika mfano nambari **1** hapo juu.

### 4.2.2 Mfumo waKonsonanti

Konsonanti ni aina ya sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo hewa kutoka mapafunikupitia chembe ya kinywa au chembe ya pua kwenda nje (Massamba na wenzake). Lahaja ya Kitumbatu ina konsonanti nyingi zikiwa ni pamoja na zile zinazounganika pamoja na kufanya sauti muambatano hasa kwa nazali na konsonanti nyengine. Konsonanti hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli Na 3 lifuatalo:

**Jedwali Na. 4.2: Konsonanti za Kitumbatu**

| **Jinsi ya kutamkwa** | | **Mahali pa matamshi** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIPASUO | | Midomo | Midomo/meno | Meno | ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | koromeo |
| | ghuna | b | | | d | | g | |
| | visoghuna | P, py | | | I | | k ky | |
| | mpunuo | ph | | | th | tʃʰ | kʰ | |
| VIZUIO KWAMIZI | ghuna | | | | | f | | |
| | visoghuna | | | | | tʃ | | |
| VIKWAMIZI | ghuna | | v | | z | | | h |
| | visoghuna | | f fy | | s | ʃ | | |
| NAZALI | | m | | | n | ɲ | ŋ | |
| VITAMBAA | | I* | | | I ly | | | |
| VIMADENDE | | | | | r | | | |
| VIYEYUSHO | | W | | | | j | | |

Chanzo:Uwandani

Katika jadweli hili, tumeona kuwa Kitumbatu kina Konsonanti ambazo hujitokeza katika matamshi ya lahaja hiyo. Sauti hizo zinaonekana katika jozi bainifu zifuatazo:-

(ɑ) **/t/ :/ k**/ :/**t**itɑ/ “mzigo wa kuni” /**k**ita/ “kuweka kizuizi”. / **t**umba /”ngisi gome” /**k**umba/ “kuzoa kwa kukusanya”.

(b) /**p**/ : / **v/:/ P**aI*a/ “pale” /val*a /”**v**aa”./**P**ungu/ “Mwanamke anyekataa kuingiliwa na mume wake”/ **V**ungu/ “nazi iliyovia”./**P**una/ “kanda sehemu iliyovunjika” /**V**una / “sega la nyuki”.

(c) /**g**/ : / **k**/ : / ko**g**ɑ/ “oga” /ko**ka/ “**washamoto”./ke**g**ɑ / “tunda lililoliwa na mnyama na kubakishwa” / ke**k**a / “ mkeka mbovu”.

(d) /**W/ / I***/ : / ko**w**a / “gamba la mgomba” / **I***o**I***a/ “oa” **./ w**ɑgo/ “ upotevu” /**I***ago / “ kambi ya uvuvi”.

(e) / **z/ / s**/ :/ tu**s**a / “lala kidogo” / tu**z**a / “tulia” . / chu**s**a / “kutoa uchungu” / chu**z**a / “ tazama” . /pe**s**a / “pepesa macho” / pe**z**a / “nyima”. / o**s**a / ‘safisha kwa maji” /o**z**a / “kugawana”.

(f) / **tʃ**/ /**f** / : / pa**tʃ**u / “ kifaa kinachotumika kupigia mbiu” / pa**f**u / “ kiungo cha mwili wa kiumbe”. / **tʃ**uza/ “tazama” /**f**uza / “fundisha”.

(g) /**I**/ **,/ j** /: / hɑle / “aina ya ngoma”, Ka**j**e /”jina la mtu”.

(h) /**r** / **/ ʃ**/ :**r**azi / “ radhi” / **ʃ**azi / “mtungo wa samaki”. / u**r**eda / “ raha” / u**ʃ**eza / “ mchezo wa watoto.

(i) / **m** / **/ h**/ : / ta**m**a / “shavu” / ta**h**a / “ tahayari”. / **m**ako / “kubeza” **/ h**ako / “hayupo”.

(j) / **n**/ /**ŋ** / : / **n**uya / “azimia” / **ŋ**uya / “nguruma”.

(k) / **p**$^{h}$/ , / **t**$^{h}$/ : / **p**$^{h}$ama / “ iba” / **t**$^{h}$ama / “shavu”.

(l) /**tʃ**$^{h}$/ , / **k**$^{h}$/ : / **tʃ**$^{h}$a / “ncha” / **kh**aa / “kaa”. / **tʃ**$^{h}$ele / “mchele kidogo” / **k**$^{h}$ele / “mtoto mdogo.

(m) **/ɬ / ɲ/ :/ ɬ**imbi / “ jogoo” /**ɲ**imbi / “nimeiba”. / **ɬ**ongwe / “ chatu” /**ɲ**ongwe / “aina ya mnyama anayeishi porini mwenye mkia mrefu.

(h) / **b** / / **d** /: /**b**aka / “doa”. / **d**aka / “kidaka cha mnazi”**./ b**akia / “rukia” /**d**alia/ “unga unaotumika kukafini maiti.

(o) **/ k**/ **,/ k**$^{h}$/ : / **k**enga / “ kuinua kichwa kwa kutazama juu”**/ k**$^{h}$enja / “ sauti kali yenye kukera”. /ni**k**a / “inamisha” /ni**k**a / “inamisha” / ni**k**$^{h}$a / “nipe”.

(p) / **P** / , / **ph** : / **P**enyuka / “kuondoka bila ya kuaga au kwa kujificha” / **Ph**enyenye / “ fununu”. /**p**iji / “Pingu ya kupandia mnazi **/ ph**ima / “ kipimo cha urefu kwa kutumia mikono ya kifua.

(q) **/ t**/ , / **th / : / t**ale / “ dafu lenye nyama laini”, / **th**agwe / “kome”. /**t**asha / “taharuki” / **th**awa / “ samaki jamii ya changu.”

(r) **/ tʃ**/ , / **tʃh** / : **/ tʃ**ombo / “jahazi” /**tʃ**$^{h}$onjo / “ tunda dogo lenye utomvu”. / **tʃ**uchia / “bembeleza mtoto**” / tʃh**u**tʃh**ua / “kumuinua mtu ili aweze kufikia kitu kilicho juu.

(s) **/ I**/ , / **I*** /**l**e**l**eja/ “fanya jambo kwa maringo” /**I***e**l**egwa / “lelewa”./ **l**ago / “rangi au tope nyeusi zinazotumika kuweka alama katika ubao” **/ I***ago /” kambi ya Uvuvi.

Vile vile, katika Kitumbatu, nazali / **m** / na/ **n** / huweza kuungana na kuunga fonimu ambatano zinazotokana na nazali kuathiri Konsonanti kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

(a) / **ng**/ , / **nj** / : / **ng**e / “nge” / **nj**e / “ nje” / bu**nj**u / “aina ya samaki mwenye sumu” / du**ng**u / “ jukwaa”.

(b) /**nd**/ , / **ng** / / ri**nd**a / “ gwaguro”, / re**ng**a / “ zunguka kama pia”.

(c) / **mb** /, / **ng** / / : / ka**mb**e / “nguo iliyochakaa” / ka**ng**e / “kifuu cha nazi kubwa”./kal*ɑ**mb**a/ “makelele ya kuomba msaada” /kal*a**ng**a/ “karara”.

Vile vile katika kitumbatu kuna muambatano wa sauti ambapo Konsonanti huambatana na viyeyusho kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:-

(a) / **fy** /,/**f** / / **fy**usa / “ rusha” / **f**usa / “viza”./**fy**aka / “ harisha” / **f**aka / “wasaa/ nafasi”.

(b) **/ Iy** / / **I*** / / ku**Iy**a / “kula” / vu**I***a / “vua”.pa**ly**a / “pale” / va**I***a / “ vaa”.

(c) / **ky**/ **/ k /** , /**ky/**, /**k**$^{h}$ / : **/ ky**uno / “ kiuno” /**k**uno / “huku”. /**ky**ungu/ “ chungu” / **k**$^{h}$ungu/ “ jamii ya mnyama paa”.

(d) **/ py**/ **,/p** / : / **py**a / “mpya” **/ p**aI*a / “paa”. /**py**eka / “bwabwatika / **p**eka / “ pekee”.

Vile vile lahaja ya Kitumbatu ina sauti / I* / . Hii ni sauti ambayo ni Kitambaza cha midomo. Hata hivyo, Maganga (1991) alibainisha sauti hiyo kama /**I**/ . Katika (uk 171) amebainisha maneno kama mu + longo [ mu**l**oŋgo] “muongo” , mu + **l**umba [mu**l**umba] “muumba”, pa + ku**l**u [paku**l**u]

“pakubwa”. Ukweli ni kwamba sauti hii / I*/ ni kitambaza cha midomo na maneno hayo hutamkwa kama [mu**l***oŋgo ] ; [mu**l***umba] , [paku**l***u] . Alama ya (*)

imetumika kutofautisha kitambaza hiki kinachotamkwa katika midomo na kile kinachotamkwa kwenye ufizi.

Naye Stude (1995) amebainisha sauti hii kama / I / yenye uvokali na ametumia alama ya nyota mbele ya neno lenye sauti hiyo kuibainisha sauti yenye uvokali imefafanuliwa kama ni Konsonanti inayotokea kati ya irabu mbili (TUKI ameshatajwa) Konsonanti hii huathiriwa na irabu inayoifuata. Hivyo alitoa mifano ifuatayo:-

a) La**l**a* “laa”
b) Ku**l**a* “kua”
c) Ka**l**anga* “kaanga”
d) Ki**l**apo* “kiapo”

Hata hivyo sauti sauti hii inaonekana kutokea katika mazingira ya mwanzo wa neno kama inavyoonekana katika maneno yafuatayo:-

a) I*al*a “lala”
b) l*ukucha “ukucha”
c) l*umiza “umiza”
d) l*uzi “uzi”

Mifano hiyo inaonesha /I / ambayo Stude (keshatajwa) ameiita yenye uvokali inaonekana ikitokea bila ya kuwa katikati ya irabu na hivyo haina sifa ya kuwa sauti yenye uvokali bali ni kitambaza cha midomo. Kitambaza hiki hukitofautisha Kitumbatu na lahaja nyengine za Zanzibar katika matamshi yake, pia kitambaza hicho hakipatikani katika Kiswahili Sanifu.

Vile vile katika Kitumbatu hakuna sauti zinazotumika katika Kiswahili Sanifu zenye asili ya Kiarabu. Sauti hizo ni nigh / **ɣ/** , dh / **ð/** , kh /**x** / , th **/ ø/.** Katika Kitumbatu, sauti hizihazijitokezi hata kwenye maneno yaliyokopwa yenye sauti hizo. Badala yake hutumia sauti za asili ya lugha kuchukua nafasi yake. Kwa mfano, maneno **gh**ali,**gh**afula,**gh**ala hutamkwa "**h**ali**, h**afla, **h**ala".Maneno kama**dh**ambi, **dh**ara, **dh**arau hutamkwa "zambi, zara, zarau". Maneno **Kh**amis, **Kh**alid hutamkwa "**h**amisi, **h**alidi". Vile vile sauti /**s/** hutamkwa katika maneno kama **th**emanini, **th**ela**th**ini hutamkwa"samanini, salasini". Hivyo tunaweza kusema kuwa lahaja ya Kitumbatu pamoja na kutumia maneno yaliyokopwa kutoka kiarabu haijaathiriwa na sauti za lugha hiyo inathibitishwa na Stigand (Keshatajwa) kuwa lahaja hii inaonesha kuwa na ubantu zaidi kuliko uarabu ukilinganisha na Kiunguja mjini.

### 4.3 Maumbo ya Maneno ya Kitumbatu

Katika kipengele hiki, mtafiti ameeleza maumbo ya maneno ya Kitumbatu kwa kuonesha namna yanavyopokea viambishi vya nafsi, njeo (wakati) na urejeshi. Pia mtafiti ameonesha maumbo ya maneno hayo jinsi yanavyokubali mnyambuliko.

#### 4.3.1 Maumbo ya Kitumbatu naViambishi Vya Nafsi

Maumbo ya maneno ya Kiswahili huwa na sifa ya kuwa na unafsi na mara nyingi hutokea katika vitenzi. Neno "unafsi" lina maana ya matumizi ya nafsi katika vitenzi vya Kitumbatu. Katika uchunguziwa hili, mtafiti amegundua kuwa vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu vina sifa ya kubeba nafsi katika hali zote, yaani katika hali ya umoja na wingi, pia katika hali ya utendaji na utendwa kama inavyoonekana kama ifuatavyo;

Katika hali ya umoja na wingi katika kauli ya utendaji na utendwa. Hii inadhihirisha kwamba vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu vinabeba sifa ya unafsi kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, kwa kuwa Kitumbatu ni lahaja, zipo tofauti chache zinazojitokeza kati ya nafsi ya  lahaja Sanifu na lahaja ya Kitumbatu. Kwa mfano :-

**Kiambishi nafsi katika utendaji (i) nafsi ya kwanza umoja na wingi**

Na- **Na**chokoka

Twa- **Twa**chokoka

Na- **Na**chuza

Twa- **Twa**chuza

**ii) Nafsi ya pili umoja na wingi**

ku- **Ku**chokoko

mu- **Mu**chokoko

ku- **Ku**chuzu

mu- **Mu**chuzu

**(iii) Nafsi ya tatu umoja na wingi**

ka- **Ka**chokoko

wa- **Wa**chokoko

ka- **Ka**chuzu

wa- **Wa**chuzu

Kutokana na mifano ya jadweli lililotangulia, tumeona kuwa katika Kiswahili Sanifu, kiambishi nafsi kiambata nafsi ya kwanza umoja na wingi huwakilishwa na **“ni’, “tu”** lakini katika lahaja ya Kitumbatu huwakilishwa na **“na”, “twa”.**Ama kwa upande wa nafsi ya pili ni kwamba Kiswahili Sanifu huwakilishwa na **“u”,”m”** wakati ambapo katika Kitumbatu huwakilishwa **na “ku” “mu”.** Kwa upande wa nafsi ya tatu, Kiswahili Sanifu huwakilishwa na **“a”, “wa**” lakini Kitumbatu huwakilishwa na **“ka”,”wa”.**

### 4.3.2 Maumbo ya Maneno naNjeo

Njeo ni kitu muhimu katika mjengeko wa maneno. Njeo huweka wazi utofauti wa wakati ambao tendo hutokea. Yaani njeo hubainisha wakati tendo linapotokea, lilipotokea na litakapotokea. Wataalamu wengi wa sarufi ya Kiswahili wamebainisha njeo katika makundi matatu ambayo ni njeo ya wakati uliopo inayowakilishwa na mofimu **“-na-”** njeo ya wakati uliopita ambayo huwakilishwa na **“-me-”** iwapo wakati uliopita ni muda mfupi na**“-li-”** iwapo wakati uliopita ni muda mrefu. Pia kuna njeo ya wakati ujao inayowakilishwa na **“-ta-”**Ama kwa upande wa lahaja ya Kitumbatu kwamba ina njeo hizo hizo kama inavyoonekana katika maelezo yafuatayo;-

**Aina ya njeo**

**Kiambishi cha njeo**

**Mfano katika uyakinishi na ukanushi**

Wakati uliopo

**-na-**

**Na**sumka ,**San**sumka

**Na**kugwa ,**San**kugwa

**Na**pakulya ,**San**pakulya

**Na**njika , **Si**nanjika

Wakati uliopita

**-me-**

**Ni**piki - **Se**pika

**Ni**pakulyu - **Se**pakulyu

**Ni**gu - **Se**kugwa

**Ni**injiki - **Se**njika

**-li-**

Wa**li**kwandika - **He**wekwandika

A**li**fyeka - **Ha**jafyeka

Mupakulyu - **He**mupakulyu

**-ta-**

Wa**ta**kwendesa - Hawa**ta**kwendesa

U**ta**lyamka - Hu**ta**lyamka

**Ta**soma - Si**ta**soma

Mifano ililopo hapo juu inabainisha njeo zilizomo katika lahaja ya Kitumbatu. Ni kuwa njeo zilizomo katika jadweli hilozinatofautianana njeo za Kiswahili Sanifu katika uyakinishi na ukanushi.

### 4.3.3 Maumbo ya Maneno ya Umilikishi

Lahaja ya Kitumbatu ina sifa ya kuwa na umilishi ndani ya maumbo ya maneno yake. Yaani, baadhi ya wakati umbo la neno hasa nomino huweza kubeba kiambishi cha umilikishi na kulifanya neno hilo lioneshe umilikishi ndani yake kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

**Shina la umilikishi**

**Mifano katika nafsi tofauti**

**Nafsi ya kwanza**

_ angu (umoja)

_etu(wingi)

Mnazi wangu

Mnazi wetu

Sahani yangu

Sahani yetu

**Nafsi ya pili**

_ ako (umoja)

_ enu (wingi)

Mnazi wako

Sahani zenu

**Nafsi ya tatu**

-ake

-ao

Mnazi wake

Mnazi wao

Katika lahaja ya Kitumbatu, umiliki katika maumbo ya maneno hujitokeza kwa kuunganishwa neno na baadhi ya silabi zinazoonesha umilikishi. Kwa mfano, katika nafsi ya tatu (umoja) mnazi wake huunganishwa pamoja na kuwa “ mtotowe” **(mwanangu, mumewe, mwanawe, mumeo)**

### 4.3.4 Maumbo ya Maneno naUdondoshaji

Katika lahaja ya Kitumbatu, udondoshaji hujitokeza katika aina nyingi za maneno kama vile katika nomino, vitenzi,vielezi, vivumishi na vihusishi kama inavyoonekana katika mifani ifuatayo:-

**Mfano wa udondoshaji katika**

**Nomino. Vitenzi, vielezi**

**Vivumishi na vihusishi.**

**Nomino**

Nchi –chi. Mfano:

Nchi ninaipenda – chi

**Kitenzi**

Ninakwenda mjini – Nda mjini

Baba ndiye mlezi - Baba ndo mlezi

Ninakwenda kula – Nda kula

**Kielezi**

Usilale chini -usilale chi

Usitupe chini - Usigele chi

**Kihusishi**

Mpunga umeliwa na kuku – mpunga uligwa n'kuku

**Kivumishi**

Kitabu chake - Kitabu che

Mifano iliygotanguliahapo juu inabainisha namna udondoshaji unavyojitokeza katika nomino, vitenzi, vielezi, vivumishi na vihusishi.

### 4.3.5 Maumbo ya Maneno Katika Uyakinishi naUkanushi

Lahaja ya Kitumbatu hubeba uyakinishi na ukanushi katika maumbo ya maneno yake. Kauli hii inathibitisha katika mifano inayoonekana katika mifano ifuatayo:-

**Hali ya uyakinishi**

**Hali ya ukanushi**

Nauka - Sinauka

Tunauka - Hatuuku

Unauka - Hunauka

Mnauka - Hamnauka

Kanauka - Hanauka

Wanauka - Hawanauka

Mifano ya hapo juu inaonesha uyakinishi na ukanushi unaojitokeza katika lahaja ya Kitumbatu katika nafsi zote tatu.

### 4.3.6 Maumbo ya Maneno naMnyambuliko

Utafiti huu umebaini kuwa maneno ya lahaja ya Kitumbatu yana sifa ya kukubali mnyambuliko kama ilivyo katika maneno ya Kiswahili Sanifu. Mifano ifuatayo inadhihirisha kauli hiyo :-

**Neno**

**i) Kukwima – kusimama**

**Kauli ya :**

**Mnyambuliko wake**

Kutenda -Kwima

Kutendwa -Kemiwa

Kutendea -Kwimia

Kutendewa -Kwimiwa

Kutendesha -Kemiswa

Kutendeana -Kwimiana

Kutendeka -Kwimika

**(ii) Kunjiika - kupika**

**Kauli ya:**

**Mnyambuliko wake**

Kutenda -Njiika

Kutendwa -Njikwa

Kutendea -Njikia

Kutendewa -Njikiwa

Kutendesha -Njikisha

Kutendeana -Njikishana

Kutendeka -Njikiiki.

**(iii) Kuronga - kuzungumza**

**Kauli ya:**

**Mnyambuliko wake**

Kutenda -Ronga

Kutenndwa -Rongwa

Kutendea -Rongea

Kutendewa -Rongewa

Kutendeshwa -Rongesha

Kutendeana -Rongeana

Kutendeka -Rongeka

Kusumka - kukimbia

**Kauli ya**

**Mnyambuliko wake**

Kutenda -Sumka

Kutendwa -Sumkwa

Kutendea -Sumkia

Kutendewa -Sumkiwa

Kutendesha -Sumkisha

Kutendeana -Sumkiana

Kutendeka -Sumkika

Mifano ya hapo juu linadhihirisha kwamba maneno ya Kitumbatu yanakubali mnyambuliko katika kauli mbali mbali. Hii ina maana kwamba mnyambuliko wa maneno ya Kitumbatu yameathiri Kiswahili Sanifu wakati wa mazungumzo.

### 4.3.7 Maumbo ya Ngeli za Nomino za Kitumbatu

Mtafiti amechunguza makundi ya ngeli za nomino za Kitumbatu na kubaini kuwa nomino nyingi ni za kawaida na hazitofautiani sana na nomino za Kiswahili

Sanifuisipokuwa baadhi ya wakati nomino za Kitumbatu huwa katika maumbo ya kilahaja na hatimaye kuyafanya makundi ya ngeli za majina kubadilika kwa kuzingatia kigezo cha upatanishi wa Kisarufi kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo :-

**Kundi A**

Mwana keshaja ( mtoto amekuja)

Wana weshaja (watoto wamekuja)

**Kundi B**

Mkono udukuku (mkono umekatika)

Mikono idukuku ( mikono imekatika)

**Kundi C**

Gino liyawa (jino limeumia)

Meno yayawa (Meno yameumia)

**Kundi D**

Kiwandazi kinjikwa (Andazi limepikwa)

Viwandazi vinjikwa ( Maandazi yamepikwa)

**Kundi E**

Ardhi ilimwa (Ardhi imelimwa)

Ardhi zilimwa (Ardhi zimelimwa)

**Kundi F**

Mchuzi usha (Mchuzi umekwisha)

Michuzi isha (Michuzi imekwisha)

**Kundi G**

Utoro umgwishi (Utoro umemfelisha)

**Kundi H**

Kwimba kunapendeza (kuimba kunapendeza)

**Kundi I**

Pahali**pa**zuri.

Mahali **mu**zuri

Kwahali **ku**zuri.

**Kundi J**

Mafuta yamwagiki.(Mafuta yamemwagika)

Tukichunguza kwa makini mifano iliyotangulia hapo juu tutagundua kuwa kila kundi linaweza kuunda kundi la ngeli fulani. Kwa mfano kundi A linaundwa ngeli ya "KE – WE" badala ya "YU – A-WA", kundi B linaunda ngeli ya "U-I", Kundi C linaunda ngeli ya "LI-YA", Kundi D linaunda ngeli ya "KI-VI", kundi E linaunda ngeli ya "I-ZI", kundi F linaunda ngeli ya "U-I", Kundi G linaunda ngeli ya "U", kundi H linaunda ngeli ya "KU", kundi Ilinaunda ngeli ya "PAMUKU" na kundi J linaunda ngeli ya "YA".

Muundo huo wa makundi ya ngeli huathiri watumiaji ya Kiswahili Sanifu wa shule Tumbatu kwa kiasi fulani kwani huwafanya wanafunzi wengi wakati wa kutunga sentensi kuingiza zaidi lahaja.

## 4.4 Tungo za Kitumbatu

Muambatano wa sauti ndio unaojenga maneno, vilevile mfuatano wa maneno ndio unaounda tungo. Kwa hivyo katika kipengele hiki mtafiti ameangalia muundo wa tungo za Kitumbatu katika hali zifuatazo:-

### 4.4.1 Tungo katika Hali ya Kiima naKiarifu

Lahaja ya Kitumbatu hubeba kiima na kiarifu katika sentensi zake. Hii ina maana kwamba lahaja hiyo inajitosheleza katika mawasiliano ya kila siku ya jamii hiyo.Ufafanuzi wa hayo unaonekana katika mifano ifuatayo:-

**Kiswahili Sanifu**

**Lahaja ya Kitumbatu**

Bibi alipakua chakula

Bibi | alipakulya chakula

K A

Daktari ameandika cheti

Daktari | kandiki cheti

K A

Mlinzi ataamka mapema

Mlinzi | katalyamka mapema

K | A

Dada anasoma kitabu

Dada | kanafyoma kitabu

K | A

Mtoto ataamka asubuhi

Mtoto | kalyamku lyunyu

K | A

Dereva ataendesha gari

Dereva | katakwendesa gari

K | A

Mifano ya tungo zilizopo hapo juu zinaonesha jinsi lahaja ya Kitumbatu inavyopokea kiima na kiarifu. Kwa hivyo, neno “bibi”, daktari, mlinzi, dada, mtoto na dereva ni viima na maneno yanayofuata ni viarifu.

### 4.4.2 Tungo za Kitumbatu naUpatanishi wa Kisarufi

Tunapochunguza tungo za lahaja ya Kitumbatu, tunaweza kubaini kuwa zina upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano, sentensi tano zilizomo katika jadwali Na 9 la hapo juu, zinabainisha kuwa zote zimepokea upatanisho wa kisarufi .

Sentensi zote hizo zinaonesha kuwa kiima chake ni mtu nafsi ya tatu ambapo kitenzi cha kiarifu chake kimeanza na kiwakilishi kiambata “Ka” ambacho ndicho kiwakilishi kinachotumika kuwakilishi nafsi ya tatu (Umoja) ya lahaja ya Kitumbatu .

## 4.5 Matumizi ya Lahaja ya Kitumbatu Darasani

Katika kubainisha jinsi lahaja ya Kitumbatu inavyotumika katika matumizi darasani, mtafiti alifika shule za Jongowe na Tumbatu na kufanya utafiti katika vipengele tofauti vya matumizi hayo. Utafiti huo uliwalenga wanafunzi nawalimu wao. Katika utafiti huo, mtafiti alitoa hojaji zenye maswali yanayohitaji majibu juu ya matumizi ya lahaja hiyo darasani kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Matini za Walimu

Mtafiti aliwaomba walimu kumpatia baadhi ya matini walizotumia katika kufundisha somo la Kiswahili kwa lengo la kuchunguza iwapo zinatumia lahaja ya Kitumbatu au hazitumii .

Katika kuchunguza matini alizopewa, mtafiti amegundua kuwa matini zote zimetumia Kiswahili Sanifu. Hali hii inadhihirisha kuwa katika maandishi ya walimu haijitokezi matumizi ya lahaja yao.

Hii ni kwa sababu kanuni ya ufundishaji inalazimisha kutumika lugha Sanifu katika maandishi, pia matini hizo ni maandishi Sanifu yaliyonukuliwa katika vitabu husika vya mada iliyokusudiwa kufundishwa. Kutokana na hali hiyo, mtafiti amebaini kuwa upo uwezekano wa walimu kufundisha kwa kutumia Kiswahili Sanifu isipokuwa hukosekana kutokana na taathira za kimazungumzo na kimazowea.

### 4.5.2 Utungaji wa Insha

Katika kuzichunguza insha za wanafunzi 22 wa shule za sekondari na 17 wa shule za msingi, mtafiti amebaini kuwa kuna matumizi ya lahaja ya Kitumbatu ingawa sio kwa kiwango kikubwa. Mtafiti ameona baadhi ya makosaya kimsamiati yaliomo ndani ya insha hizo. Mtafiti ameweza kubaini baadhi ya msamiati kama vile “chakwe” badala ya “chake” “kunako bahari” badala ya “katika bahari” “usigele”badala ya“usitupe” “uligwa”, badala ya “umeliwa”, “kanaronga”badala ya “ anazungumza” “ yawapo” badala ya “yapo”. Hiyo ni mifano ya baadhi ya misamiati ya lahaja ya Kitumbatu iliyomo ndani ya insha hizo.

Kwa upande mwengine, mtafiti alitoa maneno tofauti katika hojaji zake ili yaweze kutungiwa sentensi na wanafunzi hao. Maneno yaliotolewa ni “lima”na “soma” ambapo mwanafunzi alitakiwa kutumia njeo ya wakati uliopo (- na-), kwa neno “simama” “pika” kutumia njeo ya wakati uliopita muda mfupi (me), kwa neno “pakua”, “andika” atumie njeo ya wakati uliopitamuda mrefu (-li-), kwa neno “amka” “endesha” kwa wakati ujao (-ta-) na kwa neno “lala” “amka”kwa hali ya mazoea Katika maneno hayo, mwanafunzi alitakiwa kuyatungia sentensi katika lahaja ya Kitumbatu kisha azitafsiri sentensi hizo katika Kiswahili Sanifu.

Kwa bahati nzuri wanafunzi wote 39 waliweza kutunga sentensi katika hali zote mbili.Majibu yaliyojitokeza yaligawika katika hali tatu. Kwanza, majibu sahihi yaliyokuwa Sanifu na rasmi. Pili, majibu fasaha yasiokuwa sanifu wala rasmi na tatu majibu yaliyotumia lahaja.

**(a) Majibu sahihi yaliyokuwa Sanifu na rasmi**

Haya ni majibu yaliyotolewa na wanafunzi ambayo yamefuata taratibu zote za Kisarufi. Majibu haya yamejibiwa kwa mujibu wa njeo iliyotakiwa, yametumia nafsi sahihi iliyoungana na kiambishi awali na kitenzi, sentesi hizo zimebakia katika upatanisho wa kisarufi pamoja na kuleta maana iliyokusudiwa.

Mfano wa sentensi hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kipindupindu ni maradhi

(ii) Watu wengi hupoteza maisha

(iii) Lahaja ya Kitumbatu ina umuhimu mkubwa

(iv) Lahaja ya Kitumbatu hurahisisha mawasiliano

(v) Lahaja ya Kitumbatu ni utambulisho wa mtu

(vi) Inatupasa kudumisha usafi wa mazingira

(vii) Mwalimu ni mtu anayetoa taaluma.

Sentensi zote hizo zinaonesha kuwa pamoja na dosari za baadhi ya sentensi za wanafunzi wengine, wapo baadhi yao ambao ni hodari na wako makini sana katika matumizi sahihi ya Kisarufi. Hii inatufahamisha kuwa si wanafunzi wote wenye kuathirika na lahaja ya Kitumbatu wakati wa masomo.

**a) Majibu fasha yasiokuwa Sanifu wala rasmi**

Baadhi ya sentensi za wanafunzi zimebainika kuwa na ufasaha lakini hazikuwa sanifu wala rasmi. Neno ufasaha linaashiria kueleweka kwa sentensi hizo.

Mfano wa sentensi hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Mama anaenda kulima

(ii) Mimi nalima shamba

(iii) Mwalimu ashaandika

(iv) Dada alipakuwa ugali

Mifano hiyo inatufahamisha kuwa baadhi ya wanafunzi wanaona kuwa neno ‘anaenda”, “nalima”, “ashaandika” na “alipakuwa”ni Sanifu wakati ambapo si sahihi. Usahihi wake ni “anakwenda” “ninalima” “ameandika” na “alipakua”.

**(b) Majibu yasiyokuwa sahihi**

Mtafiti amebaini kuwa majibu mengi yasiyokuwa sahihi yamejitokeza katika njeo ya hali ya mazowea kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:-

i) Lala (Njeo ya mazowea)

- Asha hulala leo
- Hulala bibi Jumamosi
- Watoto watalala kila siku

ii) Amka (Njeo ya mazowea)

- Mgonjwa ataamka mapema
- Kila siku tumeamka asubuhi
- Watoto walitaka kuamka

Mifano hiyo inabainisha kuwa baadhi ya wanafunzi hawaelewi njeo ya mazowea wala matumizi yake.

**(c) Majibu yaliyotumia lahaja**

Mtafiti amebaini kuwa baadhi ya majibu yametumia lahaja ya Kitumbatu kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

i) Hulyalya

ii) Atakwendesa

iii) Kandiki

iv) Nakugwa

v) Usigele

Majibu hayo yanaonesha athari za lahaja kwabaadhi ya wanafunzi.Hali hiyo kwa kiasi fulani kupelekea wanafunzi hao kutofanya vizuri katika mitihani yao.

### 4.6 Athari za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu

Mtafiti amebainisha athari mbali mbali za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu. Athari hizo zimepatikana katika ukusanyaji wa data katika shule teule. Athari zilizochunguzwa ni athari za kiisimu.

#### 4.6.1 Athari za kiisimu

Mtafiti amebainisha athari za kiisimu katika sauti, maneno na tungo.

Hartman (1972) akinukuliwa na mgullu (2001) anasema kuwa Isimu ni eneo maalumu la mtalaa ambalo lengo lake ni kuchunguza lugha.TUKI (2004) imefasili isimu kuwa ni taaluma inayochunguza na kuchambua lugha kisayansi".Fasili hizo zimemwongoza mtafiti kuelewa kuwa uchambuzi wa lugha unahitaji usayansi wa hali ya juu.

#### 4.6.1.1 AthariKatika Sauti

**Jedwali Na 4.1Athari za sauti katika Kitumbatu**

| Kiswahili Sanifu | Kitumbatu | Athari |
|---|---|---|
| Alipakua | Kapaku**l**yu | Kuingia kwa sauti ya "ly" katika matamshi ya neno "alipakua" |
| Dagaa | Daga**y**a | Kuongezeka kwa sauti "y" katika matamshi ya neno "dagaa" |
| Tumempa | Tumka | Kubadilika kwa sauti "m" kuwa "k" katika matamshi ya neno "tumempa" |
| Jiwe | Ji**b**we | Kuongezeka kwa sauti "b" katika matamshi. |
| Nywele | Nyw**i**il**i** | Mabadiliko ya irabu "i" katika matamshi. |
| Nyuki | Ny**o**ki | Mabadiliko ya irabu "o"katika matamshi ya Kitumbatu. |
| Anza | Aza | Udondoshaji wa" n" katika matamshi ya Kitumbatu |
| Mguu | Mguyu | Kuingia kwa sauti "y" katika matamshi |

Katika maswali ya hojaji walioulizwa walimu na wanafunzi kulikuwa na swali linalohusiana na sauti. Swali lenyewe ni hili:

iv) Lugha ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kitumbatu katika kiwango:

A) Kikubwa ( ) (B) Kati na kati ( ) (C) Kidogo ( ) (D) Hakuna ( )

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 39 waliotakiwa kujibu, pia lilijibiwa na walimu wote 28 kati ya 29 waliotafitiwa. Majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo:

A) Majibu ya walimu

A) 7.14 %

B) 35.71 %

C) 53.57 %

D) 3.57 %

B) Majibu ya wanafunzi

A) 17.94 %

B) 30.76 %

C)30.76 %

D) 20.51 %

Mtafiti alipochunguza majibu ya walimu aligundua kuwepo kwa athari hizo katika matumizi kwa kiwango cha asilimia 95. Tukiangalia "A-B" tutaona kuwa katika kiwango hicho ni asilimia 42 ya waliokubali kwa kiwango kikubwa na kati na kati na kwa upande wa waliokubali kuwepo athari hizo kwa kiwango kidogo ni asilimia 53 wakati ambapo waliokataa ni asilimia 3.

Vile vile tukichunguza majibu ya wanafunzi tutabaini kuwa asilimia 77 inakiri kuwepo kwa athati za matumizi ya sauti za lahaja ya Kitumbatu katika somo la Kiswahili. Tumeona kuwa asilimia 47 (A –B) inathibitisha kuwepo kwa matumizi hayo katika kiwango kikubwa na kati na kati, asilimia 30 inakubali kuwepo katika kiwango kidogo ingawa asilimia 20 inasema kuwa hakuna athari hizo. Mtafiti hawezi

kupinga maoni ya wanafunzi waliokataa bali kwa kuzingatia maamuzi ya wanafunzi wengi, ameweza kukubali kuwepo kwa kwa athari hizo.

Ingawa mtafiti ameonesha kuwa athari hizo zinaonekana zaidi katika mazungumzo lakini ni wazi kuwa madhara yake hujitokeza katika maandishi.

#### 4.6.1.2 Athari katika maneno

**Jedwali Na 4.2Athari za maneno katika Kitumbatu**

| Kiswahili Sanifu | Kitumbatu | Athari |
|---|---|---|
| Utaendesha | Kuchakwendesa | Kutofautiana kwa viambishi awali nafsi ya pili umoja. Pia kutofautiana kwa njeo pamoja na shina la neno. |
| Itanyesha | Itanya | Kutumika kwa asili ya ulahaja katika msamiati wa Kitumbatu |
| Nchi | Chi | Kudondoka kwa kiambishi “N” katika lahaja ya Kitumbatu. |
| Nyinyi | Nyuye | Kubadilika kwa umbo zima la kiwakilishi |
| Buku lake | Bukulo | Kuonesha umilikishi kwa kuambatanisha nomino na kiwakilishi na kulifanya neno kuwa na umiliki ndani yake. |
| Ameanguka | Kagu | Ukosefu wa njeo ya wakati uliopita muda mfupi “me” |
| Zungumza | Ronga | Mabadiliko ya umbo katika matamshi ya Kitumbatu. |
| Usitupe | Usigele | Mabadiliko ya mzizi wa neno |

Walimu na wanafunzi waliulizwa swali kuhusu jinsi maneno ya Kiswahili Sanifu yanavyoathiriwa na lahaja ya Kitumbatu. Swali lilikuwa hivi:

v) Maneno ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika kiwango :

A) kikubwa ( ) (B) kati na kati ( ) (C) kidogo ( ) (D) Hakuna ( )

Swali hilo likuwa na lengo la kuchunguza iwapo lahaja ya Kitumbatu inaathiri maneno ya Kiswahili Sanifu. Walimu na wanafunzi walijibu swali hilo kama ifuatavyo:

i) Majibu ya walimu

A) 3.57 %

B) 39.28 %

C) 50.00 %

D)7.14 %

Tunapochunguza majibu ya walimu, tutabaini kwamba wapo baadhi yao wanaokubali kuwa lahaja ya Kitumbatu inaathiri maneno ya Kiswahili Sanifu . Tumeona kuwa asilimia 42 ndiyo iliyokiri katika kiwango “A –B” yaani kiwango kikubwa na kati na kati, asilimia 50 imekubali katika kiwango kidogo na asilimia 7 ndio iliyokataa.

ii) Majibu ya wanafunzi

A) 28.57 %

B) 20.00 %

C) 28.57 %

D) 22.85 %

kwa upande wa majibu ya wanafunzi tumebaini kuwa majibu hayo yamejitokeza katika hali mbili. Hali ya kwanza ni ile inayoonekana katika kifungu cha “A- B” kinachowakilisha kiwango baina ya kikubwa na kati na kati. Majibu haya yamechukua jumla ya asilimia 48 Hali ya pili ni ile ya “C” inayoashirikia kuwepo athari hizo katika kiwango kidogo ambayo inajumla ya asilimia 28 Majibu hayo yanaonesha athari hizo katika hali mbili. Nazo ni“hali ya umbo lenyewe” na “ulahaja uliojitokeza katika neno husika”

**(a) Hali ya umbo la neno**

Data alizokusanya mtafiti zimeonesha kuwa baadhi ya wanafunzi wameathirika na maneno ya kilahaja na kusababisha kukosekana kwa usanifu wa neno husika. Hali hii inaonekana katika mifano iliyotolewa na watafitiwa hao wakati walipotakiwa watunge sentensi Sanifu kwa kutumia maneno waliopewa kama ifuatavyo:

Maneno waliopewa

Majibu yao.

Lima – Nalima

Soma - kanasoma

Simama - Kakwima

Andika - Twankwandika

Endesha - watakwendesa

Amka - Kachaamka

Pakua - tupakulyu

Kwa kawaida, umbo la neno Sanifu hubeba viambishi vinne. Viambishi hivyo ni vya nafsi, njeo,

mzizi wa neno na kiambishi cha mnyambuliko. Neno litakalokosa mambo manne hayo hufahamika kuwa na upungufu wa kiambishi hasa kiambishi cha nafsi. Kwa mfano " nalima" badala ya "Ninalima",

Isimu ni sayansi ya lugha. Neno "usayansi" hukusanya hatua maalumu zinazomlazimu mtafiti kuzifuata katika mpangilio wake. Kutozifuata ipasavyo husababisha kupata majibu yasiyokuwa sahihi. Hivyo, ni dhahiri kuwa maneno ya hapo juu yamekosa usahihi wa kunasibishwa na nafsi yaani nafsi ya kwanza, ya pili na yatatu katika hali ya umoja na wingi.

**(b) Hali ya ulahaja iliyojitokeza katika maneno**

Ulahaja unapoingia katika neno, hujitokeza athari za kiisimu katika neno husika. Kwa mfano, mwanaisimu anapoliona neno "Nipiki", "Tupiki", "Kapiki", "Nitakwendesa", "Kuchakwendesa', "Tukwimi", "inakunya", "inyi', "itanya", "Hunya", hushindwa kufahamu kinachokusudiwa na mzungumzaji au mwandishi na kumfanya kuwa na maswali mengi akilini mwake.

Kwa hivyo, msingi wa maswali hayo ndio unaopelekea kuzuka kwa utatanishi wa tafsiri ya uchambuzi wa kazi ya viambishi vinavyojitokeza katika maneno hayo. Tafsiri ya kazi ya kila mofimu ya neno ni muhimu sana kwani ndiyo inayoongoza

katika kutoa maana sahihi inayokusudiwa.Madhara ya athari hizo hupelekea ukosaji wa natija nzuri kwa mwanafunzi hasa katika mitihani ya Taifa kwani mwanafunzi hukosa alama muhimu endapo atafanya kinyume na mwongozo wa usahihishaji uliowekwa.

#### 4.6.1.3 Athari katika Tungo

Dhana ya tungo ni pana, hivyo hukusanya mambo matatu ambayo ni kirai, kishazi, na tungo sentensi. Utafiti huu umejihusisha zaidi na mantiki ya dhana hizo ili msomaji aweze kubaini athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu zinazojitokeza ndani ya tungo za Kiswahili Sanifu. Athari hizo zimejitokeza zaidi katika kazi walizopewa wanafunzi wa msingi na sekondari katika shule husika. Kazi hizo zilikuwa ni utungaji wa Insha.

##### 4.6.1.3.1 Tungo Kirai

Kirai ni aina ya utungo wa maneno usiohusishwa na kiima na kiarifu. Wataalamu wengine wamefasili kiima kwa kusema kuwa ni neno au kifungu cha maneno kisichozingatia utendaji ndani yake. Katika kuzichunguza kazi za Insha, mtafiti amebaini baadhi ya makosa machache yaliyomo ndani ya vikundi virai vya maelezo yao kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:-

(i) Marazi ya kipindupindu

(ii) Katika mashule

(iii) Walimu wengi wa shule hii za Sekondari

(iv) Asili ya wazee wa wakati uliopita wa zamani

(v) Wakazi wa Kitumbatu

Hivyo ni vikundi virai vilivyojitokeza katikainsha zilizoandikwa na wanafunzi wa shule ya Tumbatu.Tukichunguza kwa makini Insha hizo tutabaini baadhi ya makosa ya kiisimu yaliyojitokeza katika kila kifungu. Kwa mfano katika kifungu cha kwanza kuna dosari ya kimatamshi katika neno "**marazi**" usahihi wa kimatamshi wa neno hilo ni "**maradhi**". Vile vile kifungu cha pili kina ukosefu wa upatanisho wa kisarufi ambapo wingi wa neno "**shule**" ni "**shule**" hivyo mofimu "**ma**" katika neno "**mashule**" sio sahihi. Tukichunguza kifungu cha tatu, tutabaini kwamba upo ukosefu wa mtiririko wa upatanisho wa kisarufi katika neno "**za**" inayoonesha wingi ambapo ilihitajika kutumika kihusishi " **ya**"inyonesha umoja. Ama kwa upande wa kifungu cha nne, tunabaini kuwa kuna mtiririko wa maneno yasiyohitajika kuwepo pamoja. Kwa mfano maneno **"wakati uliopita"**na **"zamani"** badala yake ilihitajika kutumika neno moja tu. Mtafiti alipochunguza kifungu cha tano alibaini kuwa ipo kasoro ya mtiririko wa upatanisho wa kisarufi katika neno "**Kitumbatu**" kwani neno hilo linaashiria kabila wakati ambapo wazo kuu katika kifungu hiki ni mahali. Kwa hivyo, usahihi wa neno hilo ni "**Tumbatu**"

Kutokana na hali hiyo, mtafiti amegundua kuwa vifungu hivyo vimejengeka zaidi kimazungumzo kuliko kimaandishi Sanifu. Hali hiyo si nzuri kwa wanafunzi wanaotarajiwa kuukabili mtihani wa taifa hapo baadaye.

#### 4.6.1.3.2 TungoKishazi

Wataalamu wengi wanakinasibisha kishazi na utendaji. Hata hivyo katika utafiti huu hatukuchunguza kishazi katika sura hiyo bali tumeangalia namna mjengeko wa tungo kishazi iliyojitokeza katika kazi za wanafunzi kama inavyoonekana katika vifungu vifuatavyo:

(i) kipindupindu husababisha kupelekea kupoteza pesa nyingi

(ii) Hatunabudi kusafisha mazingira safi

(iii) Walimu wengi wanaazibu wanafunzi.

(iv) Nawaomba jamii ya Tumbatu kulinda na kutumia Kitumbatu.

(v) Tuthamini lahaja kwani zina mchango au umuhimu mkubwa.

(vi) Utamkaji wa lahaja ya Kitumbatu hauwezi kufahamika rahisi

(vii) Mwalimu anaweza akakubalika au asikubalikwe kwa wanafunzi

Mtafiti amechunguza kwa makini vifungu hivyo na kubaini makosa ya kisarufi. Kwa kuanzia na kifungu cha kwanza, mtafiti amebaini kuwa neno "**safi**" halihitaji kuwepo kwani sentensi imeshajitosheleza kimaana. Kifungu cha pili kinaonesha kuna kosa la kisarufi linalotokana na mfuatano wa vitenzi vingi ambavyo kwa kawaida hufanya kazi ya aina moja. Hivyo neno "**husababisha**" na "**kupelekea**" hufanya kazi ya aina moja. Kwa hivyo ni vizuri neno moja kati ya hayo liondoke na hatimaye tungo isomeke " kipindupindu husababisha kupoteza pesa nyingi."

#### 4.6.1.3.3 Tungo Sentensi

Tungo sentensi huzingatia mtiririko wa neno au kifungu cha maneno chenye kuleta maana inayokamilika. Mtafiti alichunguza kazi za wanafunzi zilizowataka kutunga sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa. Katika kipengele hiki, wanafunzi wengi walitunga sentensi sahihi isipokuwa wanafunzi wachache tu. Kwa mfano, wanafunzi walipotakiwa kutunga sentensi kwa kutumia neno "lima" "soma" kwa kuzingatia njeo –**na-,** majibu ya baadhi ya wanafunzi hao walikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Miye **na**lima

(ii) Suye **twan**lima

(iii) Mwanafunzi **ka**nasoma

(iv) Weye **ku**nasoma

Mifano inaonesha mapungufu ya kiisimuyanayotokana na majibu yasiyokuwa sahihi. Miongoni mwa mapungufu hayo ni matumizi ya viambishi vya nafsi vinavyokosekana katika neno “lima” na “soma”.Matumizi sahihi ya nafsi nimuhimu sana katika isimu ya lugha kwani ndiyo inayotofautisha kati ya mtu wa kwanza, pili na tatu katika hali ya umoja na wingi hatimaye kumwezesha msomaji kumfahamu mtendaji wa tendo lilifanyika.

Vili vile, mtafiti aliwauliza walimu na wanafunzi kuhusiana na athari za tungo swali lifuatalo:

vi) Tungo za Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika kiwango:

A) Kikubwa (B) Kati na kati (C) Kidogo (D) Hakuna

Majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Majibu ya walimu

A) 0.00 % (B) 33.33 % (C) 55.55 % (D) 11.11 %

(ii) Majibu ya wanafunzi

A) 12.82 % (B) 17.94 % (C) 41.02 % (D) 28 .20 %

Tukichunguza majibu ya walimu, tutabaini kuwa idadi kubwa ya walimu imekubali kuwepo kwa athari hizo katika tungo za Kiswahili Sanifu. Idadi hiyo imekusanya jumla ya asilimia **88** ingawa kuna walimu wachache waliokataa kuwepo kwa athari

hizo kwa kiwango cha asilimia **11**. Kwa upande wa majibu ya wanafunzi ni kwamba yamegawika makundi mawili. Kundi la kwanza ni la A-C lililobeba asilimia **70** ambalo linaonesha kukataa kuwepo kwa athari hizo wakati ambapo kundi la pili ni la D lililoonesha kuwepo kwa athari hizo ambalo limebeba asilimia 28.kwa jumla tumeona kuwa majibu hayo ya wanafunzi yamepewa nguvu na majibu ya walimu na hivyo kudhihirika kuwepo kwa athari hizo ndani ya tungo za Kiswahili Sanifu.

### 4.6.2 Athari Katika Masomo Yanayofundishwa Shuleni

Mtafiti katika maswali yake ya hojaji, aliwataka watafitiwa kueleza iwapo kuna athari yoyote kwa masomo yanayofundishwa shuleni. Swali liliuliza hivi :

vii) Lahaj ya Kitumbatu huathiri masomo yanayofundishwa shuleni katika kiwango:

A) Kikubwa (B) kati na kati (C) Kidogo (D) Hakuna

Walimu na wanafunzi walijibu swali hilo kama ifuatavyo:

(i) Majibu ya wanafunzi

A) 0 % (B) 37.14 %(C) 45.71 % (D) 17.14 %

Mtafiti alipochunguza majibu ya wanafunzi, amebaini kuwa asilimia 82 ya wanafunzi 35 imekiri kuwepo kwa athari za lahaja ya Kitumbatu katika masomo yanayofundishwa shuleni.

(ii) Majibu ya walimu

A) 0 % (B) 33.33 % (C) 40.74 % (D) 25.92 %

Kwa upande wa majibu ya walimu, mtafiti amebaini kuwa asilimia 73 ya walimu 27 wamekubali kuwepo kwa athari za lahaja ya Kitumbatu katika masomo

yanayofundishwa shuleni. Hii ni dhahiri kwamba athari hizo huchangia kwa kiwango kikubwa kwa wanafunzi kutofanya vizuri katika mitihani ya taifa hasa katika masomo ya sanaa ikiwemo Kiswahili.

### 4.6.3 Athari Katika Ujifunzaji

Watafatiwa wa aina zote mbili waliulizwa swali kuhusu athari za matumizi ya lahaja hiyo katika kujifunza. Swali lilikuwa kama ifuatavyo:-

viii) lahaja ya Kitumbatu huathiri utaratibu mzima wa kujifunza kwa kiwango:

A) Kikubwa (B) Kati na kati (C) Kidogo (D) Hakuna

Jumla ya wanafunzi wote 39 na walimu 29 walijibu swali hilo. Majibu hayo yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Majibu ya wanafunzi

A)0 % (B) 41.02 % (C) 30.76 % (D) 28.20 %

(ii) Majibu ya walimu

A) 0 % (B) 27.58 % (C) 37.93 % (D) 34.48 %

Tukichunguza majibu ya wanafunzi na walimu tutabaini kuwepo kwa matumizi ya lahaja ya Kitumbatu katika ujifunzaji. Kwa kuanzia na majibu ya wanafunzi tumeona kuwa asilimia 71 inayotokana na kifungu B-C imekubali kuwepo kwa matumizi hayo. Asilimia hiyo imepata nguvu kutokana na asilimia **64** ya walimu waliokiri ambayo inatokana na kifungu cha B-C. Ujifunzaji kwa mujibu wa utafiti huu umehusisha elimu kupitia masomo tofauti yanayofundishwa katika shule hizo. Hata hivyo mkazo mkubwa wa ujifunzaji huo uko katika somo la Kiswahili. Majibu hayo

yanaashiria kwamba wanafunzi wengi wa Tumbatu hawawezi kujifunza kwa kutumia lugha Sanifu tu bali ni lazima kutumia lahaja yao kisha ndipo ifuate lahaja Sanifu. Hali hii kwa kiwango kikubwa hupelekea baadhi ya wanafunzi kushindwa kujieleza kwa kutumia Kiswahili Sanifu pekee katika kazi zao za kutunga sentensi na utungaji wa insha.

### 4.6.4 Athari katika Ufundishaji

Mtafiti aliendelea kuwauliza watafitiwa swali kuhusiana na athari za lahaja ya Kitumbatu katika ufundishaji. Wanafunzi na walimu waliulizwa swali lifuatalo:

(ix) lahaja ya Kitumbatu huathiri utaratibu wa ufundishaji kwa kiwango:

A) Kikubwa (B) Kati na kati (C) Kidogo (D) Hakuna

Wanafunzi 37 kati ya 39 walijibu swali hilo, pia walimu 21 kati ya walimu 29 walijibu. Majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Majibu ya wanafunzi

A) 2.70 % (B) 24.32% (C) 51.35 % (D) 21.62 %

ii) Majibu ya walimu

A) 0 % (B) 9.52 % (C) 57.14 % (D) 33.33 %

Mtafiti alipochunguza majibu ya wanafunzi, amebaini kwamba zipo athari za matumizi ya lahaja ya Kitumbatu wakati wa ufundishaji. Majibu haya yanaonesha kwa asilimia 77 ya wanafunzi 37 kati ya 39 waliojibu swali hilo wamekubali kuwepo kwa athari hizo. Majibu hayo yanathibitisha kuwa ufundishaji ni chanzo kikuu kinachowafanya wanafunzi wa shule za Tumbatu kuathiriwa na matumizi ya lahaja zao. Kwa upande wa majibu ya walimu, mtafiti amebaini kwamba nao wamekiri

kuwepo kwa matumizi hayo wakati wa ufundishaji. Ingawa kuna asilimia 21 ya wanafunzi na asilimia 33 ya walimu waliokataa kuwepo kwa matumizi hayo, lakini mtafiti ameona kuwa ukataaji wao hauna uzito kwa sababu idadi kubwa ya wanafunzi imekiri kuwepo kwa athari hizo, pia walimu wengi nao wamekiri kuwepo kwa matumizi hayo.

### 4.7 Sababu zilizosababisha Athari Hizo katika Kiswahili Sanifu

(i) Upungufu wa vitabu vya kujifunzia Kiswahili Sanifu shuleni. Wanafunzi wengi katika shule za Tumbatu wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa vitabu vya kujifunzia. Mara nyingi wanafunzi wanapohitaji kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu hutembelea katika maktaba za shule hizo lakini hushindwa kupata vitabu hivyo na hatimaye kuendelea kutumia lahaja yao hapo shuleni.

(ii) Uzoefu wa kutumia lugha mama. Wanafunzi wote wa shule za Tumbatu ni wakaazi wa kisiwa hicho ambao wana uzoefu mkubwa wa kutumia lahaja yao pamoja na kufanya jitihada mbali mbali za kutaka kujirekebisha kwa kutumia Kiswahili Sanifu hushindwa. Hali hiyo hupelekea matatizo makubwa kwa wanafunzi kutokana na kushindwa kufanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa kutokana na kufanya makosa mbali mbali ya kisarufi katika maandishi yao. Pia Watumbatu hufanya hivyo ili kuipa hadhi lahaja yao.

(iii) Umbali wa Kijiografia kati ya Tumbatu na Unguja mjini. Historia inaeleza kuwa Kiswahili Sanifu kinatokana na Kiunguja mjini ambacho kilisanifiwa na watumiaji wengi wa lugha hii ni wakaazi wa mjini Unguja. Kutokana na hali hiyo ni wazi kwamba masafa kutoka Unguja mjini hadi Kisiwani Tumbatu ni makubwa sana kiasi ambacho hupelekea kukosekana mwingiliano wa kazi wa

maeneo mawili hayo na hatimaye ujuzi wa kuelewa Kiswahili Sanifu hukosekana.

(iv) Muda mkubwa wa kuwepo eneo la nje ya shule. Walimu na wanafunzi wa shule za Tumabatu pia ni wakaazi wa kisiwa cha Tumbatu. Mara nyingi watafitiwa hawa hutumia muda wao mkubwa nje ya eneo la shule. Kama vile baharini, mitaani au sokoni. Maeneo yote hayo hutumika lahaja ya Kitumbatu kwa kiwango kikubwa sana hasa ukilinganisha na muda mfupi ambao wahusika hao huwepo shuleni.

(v) Kutoa ufafanuzi wa mada husika ili kuweza kufahamika kwa wanafunzi. Baadhi ya wakati walimu hutumia lahaja ya Kitumbatu darasani ili kuweza kutoa ufafanuzi wa mada kwa lengo la kuwafanya wanafunzi waelewe kwa urahisi.

## 4.8 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazozimepatikana kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano na uchunguzi shirikishi. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahasusi ya utafiti huu na umeongozwa na mkabala wa Kiidada na Usiowakiidadi. Aidha, Nadharia Kidhi ya Mawasilano iliyotumika katika utafiti huu imesaidia kuchanganua data za utafiti kwa kuchunguza mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia inayotokana na lahaja ya Kitumbatu iliyoathiri Kiswahili Sanifu, kufafanua athari za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu na kuchunguza sababu zilizopelekea kutokea kwa athari hizo.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imehitimisha utafiti unaozungumzia*“Athariza kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar”.*Sura imegawika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa utafiti mzima, sehemu ya pili inatoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu na sehemu ya tatu inaonesha mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari waUtafiti

Utafiti huu umechunguza “*Athari za kiisimu zalahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar”,* ulifanyika katika wilaya ya kaskazini “A” Unguja. Jumla ya watafitiwa **68** walishiriki katika utafiti huu wakiwemo wanafunzi na walimu wa shule za msingi na sekondari za Tumbatu na Jongowe. Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano, uchunguzi shirikishi na maktabani na zimechanganuliwa kwa mkabala wa Kiidadi na Usio wa Kiidadi. Utafiti uliongozwa na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM) ikiwa na lengo la kuchunguza athari na sababu zilizopelekea kutokea kwa athari za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar.

Hatua alizopitia mtafiti hadi akapata viambatanisho nambari i-v ni kwamba ,kwanza mtafiti alichunguza mada yake ya utafiti,kasha aliangalia lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti,maswali ya utafiti na baadae aliangalia kundi lengwa na sampuli.

Utafiti ulilenga mambo matatu. Kwanza, kuchunguza mifanyiko ya Kifonolojia na Kimofolojia inayotokana na lahaja ya Kitumbatu iliyoathiri Kiswahili Sanifu. Pili kufafanua athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu.Tatu kuchunguza sababu zilizosababisha athari hizo katika Kiswahili Sanifu. Mpangilio mzima wa kazi hii ulikuwa kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza imetoa taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti. Sura imegawika katika sehemu nane. Sehemu ya kwanza imeleza utangulizi wa sura, sehemu ya pili imeeleza usuli wa tatizo, sehemu ya tatu imeeleza tatizo la utafiti. Sehemu ya nne imebainisha malengo ya utafiti. Sehemu ya tano imetaja maswali ya utafiti. Sehemu ya sita imezungumzia umuhimu wa utafiti. Sehemu ya saba imeonesha mipaka ya utafiti na sehemu ya nane imezungumzia maadili ya utafiti.

Sura ya pili imezungumzia mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Sura imeanza kwa kuonesha maandiko kuhusu Kiswahili Sanifu, kisha sura ilieleza tafiti zinazozungumzia lahaja katika Kiswahili, baadaye ilieleza kazi tangulizi kuhusu Kitumbatu, pengo la utafiti na mwisho sura ilizungumzia mkabala wa nadharia.

Sura ya tatu imefafanua jinsi utafiti ulivyofanyika. Sura imegawanywa katika sehemu tano ambazo ni utangulizi, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji,mbinu za utafiti na mwisho imemalizia na zana za utafiti. Sura ya nne imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu na sura ya tano imetoa muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Baada ya utafiti kukamilika matokeo ya utafiti yalipatikana kupitia malengo ya utafiti.Matokeo hayo ni haya yafuatayo:

(i) Kuchunguza mifanyiko ya Kifonolojiana Kimofolojia inayotokana na lahaja ya Kitumbatu iliyoathiri Kiswahili Sanifu.

Kwanza, utafiti umebaini kuwa maumbo ya maneno ya lahaja ya Kitumbatu hutumia nafsi zenye idadi sawa na nafsi za Kiswahili Sanifu ingawa baadhi ya viambishi vinavyowakilisha nafsi hizo ni tofauti kimaumbo. Utofauti huo unajitokeza katika nafsi ya kwanza umoja na wingi, nafsi ya pili umoja na nafsi ya tatu umoja. Mtafiti amebaini kuwa Kiswahili Sanifu hutumia kiambishi "**ni**" "**tu**" cha nafsi ya kwanza umoja na wingi wakati ambapo Kitumbatu hutumia "**na**" "**twa**". Pia Kiswahili Sanifu hutumia kiambishi "**u**" cha nafsi ya pili umoja lakini Kitumbatu hutumia "**ku**". Ama kwa upande wa nafsi ya tatu umoja, Kiswahili Sanifu hutumia kiambishi "**a**" lakini Kitumbatu hutumia "**ka**"

Pili , utafiti umebaini kuwa lahaja ya Kitumbatu hutumia njeo zake katika kutambulisha nyakati ambazo tendo hutendeka. Maumbo ya njeo za Kitumbatu hayatofautiani na yale ya Kiswahili Sanifu isipokuwa kwa njeo za wakati uliopita muda mfupi na muda mrefu. Kiswahili Sanifu hutumia "**me**" kuwakilisha kiambishi njeo cha wakati uliopita muda mfupi na kiambishi "**li**" kuwakilisha njeo ya wakati uliopita muda mrefu lakini lahaja ya Kitumbatu hudondosha viambishi hivyo katika nafsi zote kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

Ni**me**pika (Nipiki),Tu**me**pika (Tupiki)

U**me**pika (Kupiki),Mu**me**pika ( Mupiki)

A**me**pika ( Kapiki),Wa**me**pika ( Wapiki)

Ni**li**pakua( Nipakulyu),Tulipakua (Tupakulyu)

U**li**pakua (Kupakulyu) ,Mu**li**pakuwa (Mupakulyu)

A**li**pakua ( Kapakulyu), Wa**li**pakuwa ( Wapakulyu)

Tatu , utafiti umebaini kuwa lahaja ya Kitumbatu huwa na sifa ya umiliki kama ilivyo katika kiswahili Sanifu isipokuwa tofauti inayojitokeza ni kwamba Kiswahili Sanifu umilikishi wake hujitokeza zaidi katika maneno mawili yaliyo mbali mbali. Kwa mfano,"Mwalimu wake" "Mtoto wake" lakini katika lahaja ya Kitumbatu umilikishi wake huonekana ndani ya neno ya moja yaani nomino huambatanishwa na kiambishi kimilikishi na kulifanya neno hilo kuwa na umiliki ndani yake. Kwa mfano, "mkewe" badala ya "mke wake" na "bukulo" badala ya "buku lako". Kwa hiyo kiambishi "**we**" cha "mkewe" na "**lo**" katika "bukulo" ndivyo inavyoonesha umilikishi.

Nne, utafiti umebaini kuwa lahaja ya Kitumbatu hudondosha viambishi katika maneno. Udondoshaji huo hujitokeza katika nomino, vitenzi, vielezi, na vivumishi kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

Nchi (nomino) : chi . Mfano chi imesaidiwa.

Ninakwenda (kitenzi) Nda.Mfano Nda mjini.

Ninakula (kitenzi) Ndala.Mfano Ndala chini.

Chini (kielezi) : chi : Nimeanguka chi.

Kitabu chake (kivumishi) : Kitabu che.

(ii) Kufafanua athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu.

Kwanza, utafiti umebaini kuwa lahaja ya Kitumbatu huathiri msamiati wa Kiswahili Sanifu kutokana na matumizi makubwa darasani. Hali hii hupelekea wanafunzi

wengi kushindwa kutumia maneno Sanifu katika mazungumzo na maandishi ya kazi zao za darasani ikiwa ni pamoja na utungaji wa sentensi na insha.

Pili, utafiti umebaini kwamba baadhi ya wakati maumbo ya maneno hutumia ulahaja. Kwa mfano neno "Amekuja" huandikwa "**keshaja**", "Umekatika" huandikwa "**udukuku"**, na "ninaendesha" huandikwa "**nakwendesa".**

(iii) Kuchunguza sababu silizosababisha athari hizo katika Kiswahili Sanifu.

Utafiti umebaini kuwa zipo sababu mbali mbali zilizosababisha athari hizo katika Kiswahili Sanifu.Miongoni mwa sababu hizo ni ukosefu wa vitabu vya kujifunzia Kiswahili Sanifu shuleni,matumizi makubwa ya lahaja ya Kitumbatu kuliko Kiswahili Sanifu, kutoa ufafanuzi wa mada

husika ili kuweza kueleweka kwa wanafunzi, umbali wa kijiografia kati ya Tumbatu na Unguja Mjini ambako hutumika Kiswahili Sanifu, muda mkubwa wa kuwepo nje ya eneo la shule na kutokuwa na ujuzi wa Kiswahili Sanifu.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa katika utafiti huu ni haya yafuatayo:

(i) Serikali kufanya utafiti wa lahaja mbali mbali kwa lengo la kuweka kumbukumbu kwa vizazi vya baadaye.

(ii) Serikali kupitia wizara ya elimu isisitize matumizi ya Kiswahili Sanifu darasani na kufuatilia utekelezaji wake.

(iii) Serikali ipeleke vitabu vya kiada na ziada vya kutosha vijijini ambavyo vitawasaidia walimu na wanafunzi kujifunza Kiswahili Sanifu.

(iv) Jamii ihamasishwe na kupewa elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa kutumia lugha fasaha.

(v) Kuanzisha vitengo maalumu vitakavyoshughulikia lahaja kwa lengo la kuzihifadhi ili zisitoweke.

## 5.5 Hitimisho

Sura hii imehitimisha utafiti unaohusu “ *Athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar”.* Sehemu ya kwanza imeeleza muhtasari wa utafiti mzima, sehemu ya pili imetoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu na sehemu ya tatu imeeleza mapendekezo ya utafiti.

## MAREJELEO

BAKIZA, (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi. Oxford University Press.

BAKIZA, (2012). Kamusi la lahaja ya Kiswahili Sanifu, Dares Salaam: Jamana Printers Ltd.

Habwe, J.na Karanja, P. (2007).*Misingi ya sarufi ya Kiswahili*.Nairobi, Printpak Ltd.

Haji, H. G. (2006).*Kamusi ya Kitumbatu Express.*Zanzibar: Printing services.

Hartman, R. K. (1972). *Dictionary of Language and linguistic,* London: Aplied Science publishers Ltd.

Kauthar, A. (2015). *Kuchunguza kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa kipemba shahadaya uzamili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Kijakazi, O. M. (2012).*Muundo wa Virai nomino katika Kitumbatu. Tasnifu ya M.A. Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Kipacha, A. (2003). Lahaja za Kiswahili, Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kitala, H. (2006). Mapitio ya ripoti ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania. Haijachapishwa, Dar-es- Salaam, Tanzania.

Kothari, C. R. (2004) Research Methods and Techniques 2nd Edition New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Kothari, C. R. (2008). Research Methodology, Methods and Techniques. New Delh: New age International Publishing Ltd.

Kothari, C. R. (2009).*Research Methodology. Methods and Techniques*, (2nd Ed), New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, D. (1990) *Research Methods,Techniques and Procedures*. Longman: University Press.

Maganga, (1991). A Study of Morphology Kiswahili, Kiunguja, Kipemba, Kimakunduchi and Kitumbatu, Dar es salaam, Tanzania.

Maganga, C. (1997).*Historia ya Kiswahili.* Dar-es-Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2007). *Nadharia ya lugha ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publisher.

Masebo, J.na Nyangwine, N. (2006).*Jitayarishe kwa Kiswahili Kidato cha 3 na 4*. Dar-es-Salaam. The General bodi Sellers Ltd.

Masebo, J. na Nyangwine, N. (2008). Kiswahili 1 kidato cha 3 na 4. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine publishers.

Massamba, D. P. (2004).*Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*.Chuo Kikuu Dar-es-Salaam, TUKI.

Mbaabu, I. (1991).*Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Mbaabu, I. (2003).“*Sheng English Dictionary: Diciphering East Africa Underworld Language*,” Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. S. (1999). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Moforojia ya Kiswahili. Dar es Salaam: Longman Publishers Ltd.

Mochuwa, Z, M. (1979). ”The impact of Kiswahili Language on ethnic Language. Acase study from Handeni District”. Tasinifu ya uzaamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Mohammed S (1984) “ Urban Versus Rurai Swahili (A Study of Pemba Varieties)”, Zanzibar (hajachapishwa). Zanzibar,Tanzania.

Msanjila, Y. P. (2006). ”Nadharia katika Isimu Jamii: Mjadala Unaoendelea Katika Mulika Na 27,TUKI:Dar es salaam kur .40-48 .

Muhura, C. (2009). *Kiswahili – Lugha na Fasihii kidato cha 3*, Dar es Salaam. Kiiya Publishers.

Mwansoko, H. J. M. (2008). “Nafasi ya Lahaja katika Kuendeleza Msamiati na Istilahi za Kiswahili Sanifu” katika kiango, J.G (mh). Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili.Dar-es-salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Nurse, D. and Hinnebuch, T. J. (1993).*Swahili and Sabaki*. Califonia: Califonia University.

Ruane, J. M. (2005).Essential of Research Methods, A Guide to social Science Research, Australia: Blackwell Publishing.

Sigh, K. (2007). Quantative Social Methods, New Delhi: SAGE Publication.

Stigand, C. (1915).“Astudy of the Morphology of Starndard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi”, Zanzibar. Haijachapwa. Zanzibar, Tanzania.

Stude, T. (1995). “Language Change and Language Maintanance on the Island of Tumbatu” (83-115) (katika Mlacha, S.A.K. na A .Hurskainen) Lugha, Utamaduni Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Tukina Idara ya Taaluma za Asia na Afrika.

TUKI, (1990).*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar-es- salaam: TUKI.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (toleo la2)* Nairobi: Oxford Universuty Press.

Walliman, N. (2011).*Research Methods: The Basic*. New York: Routdige Taylor and Francis Group.

Whitely, W. (1956) Ki- mtang'ata (A Dialect of the Mrima Coast -Tanganyika). Kampala. East African Swahili Committee.

# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho 1: Maswali ya Mtafiti kwaWalimu wa Somo la Kiswahili

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti unaohusu " *Athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika katika shule za Tumbatu Zanzibar".*

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa usahihi na kwa mujibu wa uelewa wako ili usaidie katika matokeo ya ukweli yatakayosaidia maendeleo ya Kiswahili. Majibu ya maswali haya yatakuwa siri baina ya mtafiti na mtafitiwa.

Maswali ya utafiti kwa mwalimu wa somo la Kiswahili.

1 Umri ……..Jinsia ……

2 Kazi…… Mahali pa kazi …….

3 Uzoefu wa kazi ……..Darasa unalosomesha ……

**Maswali**

1(a)unafahamunini kuhusu lahaja ?

……

……

……

b Unafahamu nini kuhusu Kiswahili Sanifu?

……

……

2 (a) Kwa kutumia sauti zifuatazo toa mfano wa nomino na kitenzi :

/a/, /b/, /c/, /d/, /e/, /f/, /g/, /h/, /i/, /j/, /k/, /l/, /m/, /n/, /o/, /p/, /q/, /r/, /s/, /t/, /u/, /v/, /w/, /x/, /y/ ,/z/

……

……

……

(b)Jee ziko sauti nyingine ambazo hazikutajwa katika jadweli lililotangulia lakini zinatumika katika lahaja ya Kitumbatu.?Zitaje pamoja na kuzitolea mifano ya maneno tofauti.

……

……

……

……

3 Tunga sentensi kwa kutumia lahaja ya Kitumbatu kwa kila njeo zifuatazo katika hali ya uyakinishi na ukanushi, kisha toa tafsiri yake kwa Kiswahili Sanifu.

Njeo ya wakati uliopo(-na-)

i. Lima

ii. Soma

sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

……

……

Njeo ya wakati uliopita

-( muda mfupi : - me-)

i. Simama

ii. Pika

sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

1. ……

2 .……

-( muda mrefu : -li- )

i. pakua

ii. Andika

sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

1. ……..

2. ……..

Njeo ya wakati ujao (-ta -)

i. Amka

ii. Endesha

sentensi

1. ……

2. ……..

Tafsiri

1. ……..

2. ……

Njeo ya mazoea (- hu-)

1. Lala

2. Amka

Sentensi

1. ……

2. ……

4. Chagua jawabu sahihi kisha weka alama ya “vema” ( √ ) ndani ya mabano.

i) Wakati wa somo la Kiswahili, matumizi ya lahaja ya Kitumbatu huwa :

a) Makubwa ( ) (b) Kati na kati ( ) (c) Madogo ( ) d) Hakuna ( )

ii. Wanafunzi huitumia lahaja yaKitumbatu wakati wa somo la Kiswahili katika Kiwango :

a) Kikubwa( ) (b) Kati na kati ( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna( )

iii. Walimu huitumia lahaja ya Kitumbatu wakati wa somo la Kiswahili katika kiwango :

a) Kikubwa ( ) (b) Kati na kati ( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna ( )

iv. Lugha ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kitumbatu katika kiwango :

a) Kikubwa ( ) (b) Kati na kati ( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna ( )

Toa mifano miwili

……

……

……

v. Maneno ya kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika kiwango :

a) Kikubwa ( ) (b) kati na kati ( ) (c) kidogo ( ) (d) Hakuna ( )

Toa mifano miwili

……

……

vi. Tungo za Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika Kiwango

a)Kikubwa ( ) (b) Kati na kati ( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna ( )

Toa mifano miwili

……

……

vii. Kwa maoni yako eleza sababu tatu zilizopelekea kutokea kwa athari hizo

1. ……

2. ……

3. ……

**AHSANTE KWA MASHIRIKIANO NA MSAADA WAKO.**

**Kiambatanisho 2: Maswali ya Mtafiti kwaWanafunzi wa Shule za Msingi naSekondari**

**Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa ufahamu wako:**

1 Umri ……..Jinsia ……

2 Kazi …… Mahali pa kazi …….

3 Mahali unapoishi …….. Darasa unalosoma ……

**Maswali**

1(a)unafahamu nini kuhusu lahaja ?

……

……

b Unafahamu nini kuhusu Kiswahili Sanifu?

……

……

2( a) Kwa kutumia sauti zifuatazo toa mfano wa nomino na kitenzi :

/a/, /b/, /c/, /d/, /e/, /f/, /g/, /h/, /i/, /j/, /k/, /l/, /m/, /n/, /o/, /p/, /q/, /r/, /s/, /t/, /u/, /v/, /w/, /x/, /y/ ,/z/

……

……

……

b Jee ziko sauti nyingine ambazo hazikutajwa katika jadweli lililotangulia lakini zinatumika katika lahaja ya Kitumbatu.?Zitaje pamoja na kuzitolea mifano ya maneno tofauti.

……

……

……

3 Tunga sentensi kwa kutumia lahaja ya Kitumbatu kwa kila njeo zifuatazo, kisha toa tafsiri yake kwa Kiswahili Sanifu.

Njeo ya wakati uliopo(-na-)

i. Lima

ii. Soma

sentensi

1. ……

2. …….

Tafsiri

1. ……

2. ……..

Njeo ya wakati uliopita

-( muda mfupi : - me-)

i. Simama

ii. Pika

sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

1. ……

2. ……

-( muda mrefu : -li- )

i. pakua

ii. Andika

sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

1. ……

2. ……

Njeo ya wakati ujao (-ta -)

i. Amka

ii. Endesha

sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

1. …….

2. ……

Njeo ya mazoea (- hu-)

1. Lala

2. Amka

Sentensi

1. ……

2. ……

Tafsiri

……

……

4 Chagua jawabu sahihi kisha weka alama ya “vema” ( √ ) ndani ya mabano.

i) Wakati wa somo la Kiswahili, matumizi ya lahaja ya Kitumbatu huwa :

a) Makubwa ( ) (b) Kati na kati ( ) ( c) Madogo ( ) (d) Hakuna ( )

ii. Wanafunzi huitumia lahaja ya Kitumbatu wakati wa somo la Kiswahili katika Kiwango :

a) Kikubwa( ) (b) Kati na kati( ) (c) Kidogo( ) (c) Hakuna( )

iii. Walimu huitumia lahaja ya Kitumbatu wakati wa somo la Kiswahili katika kiwango :

a) Kikubwa ( ) (b) Kati na kati( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna( )

iv. Lugha ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kitumbatu katika kiwango :

a) Kikubwa ( ) (b) Kati na kati ( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna( )

Toa mifano miwili

……

……

v. Maneno ya kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika kiwango :

a) Kikubwa ( ) (b)kati na kati( ) (c) kidogo ( ) (d) Hakuna( )

Toamifano miwili

……

……

vi. Tungo za Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika Kiwango

a) Kikubwa( ) (b) Kati na kati( ) (c) Kidogo ( ) (d) Hakuna( )

Toa mifano miwili

……

……

vii. Kwa maoni yako .eleza sababu tatu zilizopelekea kutokea kwa athari hizo.

1. ……

2. …….

3. ……

**AHSANTE KWA MASHIRIKIANO NA MSAADA WAKO**

**Kiambatanisho 3: Matini ya mwalimu wa somo la Kiswahili**

**Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa ufahamu wako:**

1 Umri …….. Jinsia ……

2 Kazi …… Mahali pa kazi …….

Uzoefu wa kazi …… Darasa unalofundisha ……

Ninaomba uniandikie matini yako ulioiandaa kwa ajili ya wanafunzi wako wa somo la Kiswahili.

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

**AHSANTE KWA MASHIRIKIANO NA MSAADA WAKO**

**Kiambatanisho 4: Utungaji waInsha kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekomdari**

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa ufahamu wako:

Umri …….

Jinsia…….

Kazi ……..Pahala pa kazi ……..

Mahali unapoishi ……Darasa unalosoma ……..……

Tunga insha isiyopungua maneno 100 kati ya moja ya mada zifuatazo :-

1. Maradhi ya kipindupindu 2. Mwalimu ninayempenda

3. Umuhimu wa lahaja ya Kitumbatu.

……

……

……

……

……

……

……

……

**AHSANTE KWA MASHIRIKIANO NA MSAADA WAKO**

**Kiambatanisho 5: Maswali ya Mahojiano**

**Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa ufahamu wako:**

1. Kwa mujibu wa ufahamu wako ninaomba uniambie tofauti zilizopo kati ya lahaja na Kiswahili Sanifu.

2 (a). Naomba unitajie sauti za lahaja ya Kitumbatu.

b. Kwa kutumia sauti hizo, toa mifano ya nomino na vitenzi.

3 (a).Unafahamu nini kuhusu njeo?

b. Kwa kutumia njeo hizo, naomba kwa ridhaa yako utunge sentensi kwa lahaja ya Kitumbatu kisha toa tafsiri yake kwa Kiswahili Sanifu.

4. Ninaomba unipatie mifano ya maumbo ya maneno ya lahaja ya Kitumbatu katika hali zifuatazo:-

i) Umilikishi (ii) Ukanushi (iii) Uyakinishi (iv) Mnyambuliko na (v) Udondoshaji.

5. Kwa kutumia lahja ya Kitumbatu, naomba unipatie mifano tofauti ya ngeli za nomino.

6. Geuza sentensi zifuatazo kwa lahaja ya Kitumbatu:-

i) Mtoto amekuja.

ii) Mkono umekatika.

iii) Jino limetoka.

iv) Kitabu chake kimepotea.

v) Ardhi imelimwa.

vi) Utoro umemfelisha.

7. Jee, walimu na wanafunzi hutumia lahaja ya Kitumbatu wakati wa somo la Kiswahili darasani.?

8. Tafadhali nitajie athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu kinachotumika hapa shuleni.

9. Naomba unitajie sababu tatu zilizosababisha athari hizo katika Kiswahili sanifu.

10. Toa mapendekezo yako kuhusiana na nini kifanyike katika kuondoa athari hizo.

**AHSANTE KWA MASHIRIKIIANO YAKO**